JACKPOT BABA LAO!
TZS. 367,741,460
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Askari** afariki dunia akilinda mtihani wa taifa

UKURASA 3



**MWIJAKU, HARMONIZE HAWAPIKIKI TENA**

UKURASA 20


# Nipashe JUMAPILI

Jumapili Oktoba 9, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0581093

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US




# Corona bado tatizo nchini

• **Wagonjwa** wapya 470 wagundulika.... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO


**UKURASA WA 5**

### UKAGUZI LESENI 40,000 ZA MADINI KURINDIMA

TUME ya Madini imesema mwaka huu inatarajia kufanya tathmini na ukaguzi wa leseni za madini zaidi ya 40,000 zilizopo ili kuzifuta ambazo...

**UKURASA WA 8**

### WAKAIDI TAHADHARI YA EBOLA KUFUNGIWA BIASHARA ZAO

SERIKALI imesema itafunga biashara za wafanyabiashara ambao watakaidi kuweka vifaa vya kujikinga na tishio la...

**UKURASA WA 17**

### MBUNGE ASIMAMISHWA KISA NYWELE ZA FARAGHA

MBUNGE mmoja nchini Zambia amepewa adhabu ya kusimamishwa kazi kwa muda wa mwezi mmoja baada ya kutaja nywele za sehemu...






Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Biashara Tanzania (TCB), Sabasaba Moshingi (wa pili kushoto), akionyesha ishara ya ushujaa na wanachama wa kikundi cha wajasiriamali wanawake cha Furahia Women Cooperative, kabla ya kukabidhi kisima cha maji safi kwa Mbunge wa Paje, Sudi Hasani, kilichojengwa na benki hiyo kwa ajili ya kikundi hicho wilayani Kusini Unguja mwishoni mwa wiki, ikiwa ni sehemu ya kuadhimisha kilele cha Wiki ya Huduma kwa Wateja. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Minada korosho yaiva

UKURASA 4

## Mabilioni ya serikali hatarini kupotea mtaani

UKURASA 2

**MICHEZO** YANGA, AL HILAL HAKUNA MBABE UK.24 | **MAONI, KATUNI** UK.6




Mwenyekiti wa Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA), Joyce Shebe (wapilikulia), akiwa katika picha ya pamoja na wajumbe wapya wa Bodi ya TAMWA, jijini Dar es Salaam juzi, wakatiwa kikao kazi cha siku mbili cha kuwaandaa kuanza majukumu yao. Wajumbe wapya wa Bodi ni Mary Hospicia Kafyome, Dk. Kaanaeli Kaale, Asha Abdi Makame, CPA Caroline Mdundo, Dk. Rukaya Wakif Muhammed na Wakili Annuciater Charles Bulashi. **PICHA: TAMWA**

# 470 wapata maambukizi UVIKO-19, Dar yaongoza

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WATU 478 wamethibitika kuwa na maambukizi ya UVIKO-19 ndani ya kipindi cha miezi mitatu huku Mkoa wa Dar es Saalam ukiwa na idadi kubwa zaidi ya wagonjwa.

Vilevile, tangu kuanza kutolewa kwa huduma za chanjo ya UVIKO-19 nchini, jumla ya wananchi milioni 22.09 wamepata dozi kamili ya ugonjwa huo kati ya milioni 30.74 waliotarajiwa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mganga Mkuu wa Serikali Dk. Aifello Sichalwe kwa vyombo vya habari, serikali kupitia Wizara ya Afya imeendelea kuimarisha mapambano dhidi ya UVIKO-19 nchini na kutoa taarifa kwa umma kuhusu mwenendo wa ugonjwa huo.

"Katika kipindi cha kuanzia Agosti 26 hadi Oktoba 7, 2022, jumla ya watu 478 wamethibitika kuwa na maambukizi ya UVIKO-19 kulinganishwa na watu 586 kwa kipindi cha mwezi mmoja uliopita kuanzia Julai 30 hadi Agosti 26, 2022, hivyo kasi ya maambukizo kupungua kwa asilimia 18.4.

Katika taarifa yake hiyo, Dk. Sichalwe alibainisha kuwa katika kipindi hicho, hakukuwa na vifo kulinganisha na kipindi cha Julai 30 hadi Agosti 26, 2022 ambacho kilikuwa na vifo vinne vilivyoripotiwa kutokana na UVIKO-19.

Alisema mchanganuo wa takwimu katika kipindi cha Agosti 27 hadi Oktoba 7, 2022, unaonyesha watu waliothibitika kuwa na ugonjwa huo walitoka katika mikoa 17.

Aliitaja mikoa hiyo pamoja na idadi ya wagonjwa kwenye mabano ni Dar es Salaam (382), Mwanza (28), Arusha (23), Mara (8), Dodoma (5), Manyara (5), Morogoro (5), Lindi (4), Mbeya (4), Singida (3), Pwani (2), Kigoma (2), Katavi (2), Ruvuma (2), Mtwara (1), Kilimanjaro (1) na Tanga (1). Alisema jumla ya wagonjwa wanne waliothibitika kuwa na UVIKO-19 walilazwa na wote walikuwa hawajapata chanjo ikiwa ni kupungua kwa wagonjwa wanne kulinganisha na wagonjwa wanane waliotolewa taarifa kwenye tamko lililopita.

Alisema serikali imeendelea kutoa huduma za chanjo ya UVIKO-19 nchini ili kuwawezesha wananchi kupata kinga dhidi ya ugonjwa huo.

Alisema kuwa kuanzia Agosti 27 hadi Oktoba 7, 2022, wananchi 3,499,099 wenye umri wa miaka 18 na kuendelea walipata dozi kamili ya chanjo ya UVIKO-19 ikiwa ni kupungua kwa asilimia 10.3 kulinganisha na watu 3,902,839 waliopata dozi kamili katika wiki ya tarehe Julai 30 hadi Agosti 26, 2022.

"Ndugu wananchi, tangu chanjo za UVIKO-19 zimeanza kutolea mpaka kufikia Oktoba 7, 2022, jumla ya wananchi waliopata dozi kamili ni 22,098,872 kati ya watu 30,740,928, sawa na asilimia 71.89. Lengo ni kuchanja asilimia 100 ya Watanzania wote wenye umri wa miaka 18 na kuendelea," alisema.

Kiongozi huyo wa serikali alisema wizara inaendelea kuwahimiza wananchi kupata na kukamilisha dozi za chanjo ya UVIKO-19 ili kuzuia kupata ugonjwa mkali hata kifo, pale mtu anapopata maambukizi.

Alisema wizara inatoa tahadhari kwa wananchi wote kuendelea kuchukua hatua za kujikinga na UVIKO-19 ikiwa ni pamoja na kupata kwa wakati dozi kamili za chanjo ya UVIKO-19.

"Kuvaa barakoa pindi unapojisikia dalili za mafua ili kuzuia kusambaa kwa maambukizi, kuzingatia usafi binafsi ikiwamo kunawa mikono mara kwa mara kwa maji tiririka na sabuni au kutumia vipukusi (sanitizer), kuwahi kwenye vituo vya kutolea huduma za afya endapo utakuwa na dalili za ugonjwa huu," alisisitiza.

Pia aliwataka Watanzania kuendelea kuchukua hatua za kujenga mwili kwa kufanya mazoezi na kula vyakula bora na kutoa taarifa za kuwapo watu wenye dalili za ugonjwa huo katika jamii kupitia namba ya simu ya bure 199.

# Mabilioni ya umma yalivyo hatarini kupotelea mitaani

**Na Sabato Kasika**

MWENYEKITI wa Huduma za Jamii Manispaa ya Ubungo, Edward Laiza amebainisha kuwa hadi kufungwa kwa mwaka fedha wa 2021/22, zaidi ya Sh. bilioni 2.8 za marejesho ya mikopo kwa makundi maalum (wanawake, vijana na watu wenye ulemavu) zilikuwa hazijarejeshwa katika halmashauri hiyo.

Laiza alibainisha hayo wakati wa mkutano kuhusu mrejesho wa ufuatiliaji wa bajeti ya Kata ya Saranga ulioandaliwa na Kituo cha Taarifa na Maarifa cha Kata hiyo ambacho kiko chini ya Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP).

"Hadi tunafunga mwaka wa fedha wa 2021/22, zaidi Sh. bilioni 2.8 zilikuwa hazijarejeshwa na vikundi mbalimbali vilivyokopeshwa na manispaa yetu, hali ambayo inasababisha wengine washindwe kukopeshwa," alisema Laiza.

Mwenyekiti huyo alisema manispaa inaendelea kufuatilia fedha, huku akivitaka vikundi vilivyokopa fedha katika manispaa hiyo vihakikishe vinarejesha.

"Pamoja na changamoto ya urejeshwaji wa mikopo, wanawake wameonyesha uaminifu wa hali ya juu katika urejeshwaji huo, si wasumbufu, hivyo ingekuwa vyema kama wengine mtajifunza kwao," alishauri.

Laiza ambaye pia ni Diwani wa Saranga alielezea kukwama kwa mikopo hiyo mikononi mwa vikundi ikiwa ni miezi sita tangu viongozi wa manispaa walipokutana kujadili sakata hilo.

Machi mwaka huu Idara ya Maendeleo ya Jamii Manispaa ya Ubungo ilikutana na Ofisa Utumishi Mkuu wa Manispaa hiyo, Selemani Kateti kujadili mikakati ya kufuatilia na kupata marejesho ya mikopo iliyotolewa kwa vikundi hivyo na kuwasilisha taarifa ya hali ya mikopo hiyo kwa kila kata.

Uamuzi huo ulichukuliwa kwa kuzingatia taarifa ya hali ya utoaji na urejeshwaji wa fedha za mikopo hiyo ambayo inaonyesha kuwa kwa kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2017/18 hadi 2021/22, halmashauri ilitoa Sh. bilioni 6.7 za mkopo lakini kufikia Machi mwaka huu ni Sh. bilioni 1.97 tu zilizokuwa zimerejeshwa, huku Sh. bilioni 4.79 zikiwa mikononi mwa vikundi.

Kaimu Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii wa Manispaa hiyo, Mercy Ndekeno alisema wanafuatilia kwa karibu, akisisitiza idara ilikuwa imeazimia kuendelea kuchukua hatua kwa wanavikundi wanaokaidi kurejesha mikopo hiyo kama sheria za manispaa zinavyoelekeza.

Alitaja moja ya hatua hizo ni kufanya vikao vya mara kwa mara kujadili utekelezaji wa kazi hiyo kwa kushirikiana na watendaji wa kata na mitaa.

Ofisa Utumishi Kateti aliwahimiza maofisa hao kushirikiana vyema na viongozi wote wa kata na mitaa, ili kuongeza ufanisi katika kupata marejesho ya mikopo hiyo na kuvitembelea vikundi vya kata kila mara.

Wakati Ubungo kukiwa na hali hiyo, mwanzoni mwa mwaka huu, Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegelo aliiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuwachukulia hatua waliotajwa kuhusika katika ubadhirifu wa fedha za mikopo hiyo itokanayo na asilimia 10 ya mapato ya halmashauri.

Jokate aliagiza hayo baada ya kamati aliyoiunda kufuatilia mikopo hiyo kubaini 'madudu' katika utoaji wa mikopo hiyo, yakijumuisha usajili wa vikundi kuwa na mwingiliano wa namba za usajili ambapo namba moja inatumika kwa zaidi ya kikundi kimoja.

Mengine ni vikundi kupewa mkopo kabla havijapitishwa katika kikao cha ngazi ya kata, kutofuata utaratibu wa uombaji wa mikopo, baadhi ya vikundi kuundwa kiujanjaunja, huku baadhi ya wajumbe wakitoka nje ya kata husika.

Vilevile, baadhi ya watendaji wa kata na maofisa maendeleo wa kata wanatuhumiwa kubadilisha mihutasari ya vikao vya baraza la kata, ili kuongeza majina ya vikundi wanavyotaka kuvipatia mikopo kinyemela.

Lingine ni baadhi ya wanufaika ya mikopo kuwa watumishi wa serikali au watu wenye ajira rasmi, lakini pia baadhi ya wanufaika kunufaika kwa wakati mmoja katika kata tofauti.

Baadhi ya fedha zilizotolewa kwa baadhi ya vikundi zimeshindwa kuanzisha miradi iliyokusudiwa kutokana na fedha hizo kutolewa na kumlipa mzabuni hewa aliyeshindwa kuwasilisha bidhaa za mradi wa kikundi.

Tuhuma nyingine ni baadhi ya vikundi vilivyopewa mikopo kutokuwa na mkataba unaovibana kurejesha mikopo hiyo, kitendo ambacho kimetokana na manispaa kutokamilisha kwa wakati utiaji saini mikataba ya vikundi, huku vikundi vingine vikipewa mikopo nje ya shughuli wanazofanya.

Kukwama kwa mikopo mikononi mwa baadhi ya vikundi ni tatizo ambalo limekuwa likitatuliwa na kuibuka kama ambavyo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) amekuwa akiliibua katika ripoti zake za ukaguzi.

Kwa mujibu wa ripoti zake, katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2020/21 iliyowasilishwa bungeni Aprili 12 mwaka huu, CAG Charles Kichere anabainisha halmashauri 155 hazikukusanya Sh. bilioni 47.01 za marejesho ya mikopo iliyotolewa kwa makundi hayo.

Ikirejewa historia ya utoaji wa mikopo hiyo ilianzia mwaka 1993 serikali ilipoanzisha Mfuko wa Fedha wa Maendeleo kwa Wanawake na Vijana ili kuwainua wanawake na vijana wasiojiweza kiuchumi ambapo wengi wao hawakidhi vigezo vya mikopo inayotolewa na taasisi za fedha kutokana na ukosefu wa dhamana.

Kwa wakati huo, mikopo hiyo ya uwezeshaji ilitolewa asilimia tano kwa wanawake na asilimia tano kwa vijana.

Mwaka 2019, serikali kupitia Bunge, ilirekebisha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290 kwa kuongeza kifungu cha 37A mahususi kwa ajili ya kuwezesha mikopo kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

## Bil 4.5/- kunufaisha wakulima wa alizeti

**Na Beatrice Moses**

MRADI wa Sh. bilioni 4.5 unaotekelezwa na Taasisi ya Kuboresha Mifumo ya Masoko ya Kilimo Tanzania (AMDT), unatarajia kuwanufaisha wakulima 100,000 wa mazao ya alizeti na mikunde walioko kwenye mikoa 11.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mkoani Dar es Salaam, Mtendaji Mkuu wa AMDT, Charles Ogutu, alisema fedha hizo zitatolewa kama ruzuku kwa taasisi za serikali na mashirika wabia ambao wataongoza utekelezaji wa miradi kwenye mikoa hiyo.

Alisema uwekezaji huo mkubwa unalenga kusaidia kwenye vipaumbele vya serikali katika sekta mama ya kilimo kama ilivyoainishwa kwenye ajenda 10/30 na programu ya kuendesha sekta ya kilimo ASDP 11.

"Uwekezaji huu unalenga kuwawezesha wakulima kupata mbegu bora, kuunganishwa na huduma za biashara na fedha katika minyororo ya thamani ya alizeti na mikunde.

"Pia kuboresha huduma za ugani, usimamizi wa mavuno na uchakataji wake na kuongeza thamani ya mazao haya, mikoa itakayonufaika ni Manyara, Singida, Morogoro, Dodoma, Lindi, Arusha Ruvuma, Songwe, Rukwa na Njombe," alisema.

Aliongeza kuwa miradi hiyo itatekelezwa hadi mwaka 2023 na endapo itakuwa na mafanikio, itaongezwa muda hadi mwaka 2024.

Ogutu alisema miradi hiyo itatekelezwa kwa kuzingatia masuala ya usawa wa jinsia na mbinu za kukabialiana na mabadiliko ya hali ya hewa.

Pia alisema wanatarajia kufanya hamasa ya ulaji wa mazao ya kunde ikiwamo mbaazi, ambazo zimethibitishwa hupunguza udumavu wa akili.

Mkurugenzi Mkazi wa Farm Africa, Mary Batterman alisema ni muhimu mkulima wa alizeti kupata mbegu bora kwa kuwa huinua kipato kutokana na mavuno mazuri yanayopatikana.

Mratibu wa alizeti kitaifa kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Frank Reuben alisema mahitaji ya mbegu bora ya alizeti ni mara 10 ya mbegu zinazozalishwa.

"Kuna fursa kubwa kwa kampuni za ndani na nje ya nchi kuwekeza katika eneo hili ili kuwezesha kupatikana kwa wingi mbegu bora kulingana na mahitaji yaliyopo," alisema.

# Askari alivyofariki dunia akilinda mtihani wa taifa

**Na Steven William,** MUHEZA

ASKARI wa Jeshi la Akiba (Mgambo), mkazi wa Kijiji cha Manyoni, Kata ya Misozwe wilayani Muheza mkoani Tanga, Yustino Mhina, amekutwa amefariki dunia kwenye kiti wakati akilinda mtihani wa darasa la saba mwaka huu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Henry Mwaibambe, alithibitisha jana kutokea kwa kifo hicho, akibainisha kuwa askari huyo alikutwa na umauti Alhamisi ya wiki hii, siku ya pili ya mtihani huo wakati watahiniwa wa darasa la saba wakifanya mtihani huo wa kuhitimu elimu ya msingi.

Alisema Mhina alikuwa akilinda mtihani huo katika Shule ya Msingi Lumbizi iliyoko Kijiji cha Kwatango, Kata ya Kwemingoji wilayani hapa.

Kaimu Ofisa Mtendaji wa Kata ya Kwemingoji, Levina Mushi, alisema askari huyo ambaye tayari mwili wake umeshazikwa, alibainika kupoteza maisha wakati walinzi wenzake walipomkuta asubuhi akiwa kwenye kiti shuleni huko.

Mtendaji huyo alisema mwili wake ulipelekwa Hospitali Teule ya Wilaya ya Muheza kwa ajili ya uchunguzi na majibu yalionyesha alikunywa dawa zaidi ya kipimo.

Alisema mlinzi huyo alikuwa anasumbuliwa na maradhi ya kifafa na alikuwa anatumia dawa kutibu ugonjwa huo.



Mafundi wa Kampuni ya Skol, wakiendelea na ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua kwenye barabara ya Buza Kanisani, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Serikali kuongeza mashine za upasuaji kukabili Ebola

**Na Mary Geofrey,** KAGERA

KATIKA kukabiliana na ugonjwa wa Ebola nchini, Wizara ya Afya inatarajia kuongeza mashine ya usingizi na upasuaji katika kituo maalum cha matibabu ya wagonjwa watakaobainika kuwa na Ebola kwenye Kituo cha Afya Kabyaile wilayani Misenyi mkoani Kagera.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu alibainisha hayo juzi, akimwelekeza Mganga Mkuu wa Mkoa huo, Issessanda Kaniki kuhakikisha vifaa tiba hivyo vinafika kituoni huko ndani ya siku saba kutoka Bohari ya Dawa (MSD) ambako vimeagizwa.

Ummy alitembela kituo hicho kuangalia maandalizi yaliyofanyika na utayari wa watoa huduma wa kupokea wagonjwa endapo ugonjwa huo utaingia nchini.

"Serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa upande wa huduma za afya inajikita kwenye ubora wa huduma, hivyo vifaa tiba tutaleta hapa, maana yake atakapotokea mgonjwa wa Ebola na anatakiwa kufanyiwa upasuaji tutafanya hapa hapa, maana tutampeleka wapi kama hatuna vifaa?" alihoji.

Waziri Ummy aliwahimiza wananchi walio jirani na kituo hicho kukata Bima ya Afya kwa Wote (UHC) ambayo itawaondolea gharama za matibabu na malalamiko ya kuchangia huduma za tiba pindi wanapougua.

"Bima ya afya kwa wote itatuondolea malalamiko haya ya kuchangia, hatutampiga faini mtu yeyote, bali tutawahamasisha kila Mtanzania kuwa na bima ya afya," alisema.

Waziri Ummy pia aliwakumbusha wananchi hao kuendelea kuchukua tahadhari zote za kinga ikiwamo kunawa mikono mara kwa mara kwa maji tiririka na sabuni, kuepuka kugusa, damu, matapishi, kamasi, mate, machozi, mkojo, kinyesi na majimaji mengine yanayotoka mwilini mwa mtu mwenye dalili za Ebola.

**FOMU MIRATHI-2**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Kihonda**
**Wilaya ya Morogoro**
**Mkoa wa Morogoro**
**Usimamizi wa Mirathi Na 52 / 2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU HALIMA JUMA MARA WA MOROGORO MJINI**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA ALLY HAMISI SALEHE**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote / maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 13/10/2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo

**Zingatia;**

Endapo kuna yoyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.

* Wosia wa Marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
* Marehemu hakuacha wosia
* Futa isiyohusika

**Imetolewa leo tarehe 06/10/2022**

HAKIMU
HAKIMU
MOROGORO

# Minada ya korosho kuanza wiki ijayo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MINADA ya mauzo ya korosho kwa msimu huu itaanza Oktoba 14 mwaka huu huku wakulima wakitolewa hofu kuhusu bei.

Akizungumza jana jijini hapa, Kaimu Mkurugenzi wa Bodi ya Korosho Tanzania, Francis Alfred, alisema mwaka huu wamepanga kuzalisha tani 400,000 za korosho na mfumo utakaotumika utakuwa wa stakabadhi ghalani.

"Hali ya soko kwa ujumla kulingana na soko la dunia ipo vizuri, tuwatoe wasiwasi wakulima hali ya soko ni nzuri na tuna imani watapata thamani ya mazao yao watakapouza katika msimu unaoanza," alisema.

Aliwataka wakulima katika vyama vya msingi na vyama vikuu waanze kufungua na kukusanya korosho kwenye vyama hivyo.

"Bodi ya usimamizi wa ghala waanze kufungua maghala ili wakulima wakikusanya kwenye vyama vya msingi, zipelekwe ghalani ili lengo letu la kuanza Oktoba 14 mwaka huu lifanikiwe," alisema.

Kaimu Mkurugenzi huyo alisema wameweka mkakati kuhusu vifungashio vya magunia ambapo wanahitaji magunia 500,000 ili kukabiliana na tatizo la vifungashio.

"Kumekuwa na changamoto kubwa ya ukosefu wa vifungashio kila msimu, lakini hadi sasa kuna magunia ambayo yanatosha kuweka korosho tani 345,000 na tumesambaza na suala la vifungashio kwa mwaka huu hatuna changamoto kabisa.

"Tumeenda mbali zaidi suala la ufuatiliaji kwa hiyo magunia yote yatakayoweka korosho mwaka huu yatakuwa na nembo ya chama kikuu, alama ya chama cha msingi. Kwa hiyo, korosho yoyote itakayokwenda ghala kuu inajulikana chama kikuu gani na AMCOS ipi," alisema.

Alisema kama likikutwa gunia India na watakuwa na uwezo wa kufuatilia kujua korosho hizo zilikotoka.

"Tumesema hakuna gunia litakaloweka korosho kama halijawekwa hizo alama," alionya.

Pia alisema bodi tayari imeanza kusajili na kutoa leseni kwa wanunuzi wa korosho ghafi kwa ajili ya kusafirisha nje ya nchi na kubangua nchini.

"Hadi kufikia Oktoba 7 mwaka huu, kampuni 48 zimejisajili na kati yake kampuni 18 tayari zimepata leseni na zilizosalia zipo hatua mbalimbali za kukamilisha upataji wa leseni,"alisema.

Aliongeza kuwa kwa sasa wanasajili wakulima na lengo ni kusajili wakulima 400,000. Alibainisha kuwa hadi sasa wamesajiliwa wakulima 281,000.

Alisema asilimia 90 ya korosho inayouzwa ni ghafi, hivyo bodi imedhamiria kuongeza ubanguaji wa korosho ambao kwa sasa upo chini ya asilimia 10.

"Upanguaji upo chini ya asilimia 10 ya uzalishaji, tani 30,000 zinatarajiwa kubanguliwa nchini. Kati yake, tani 400,000 zinazotarajiwa kuzalishwa, tunadhamiria ubanguaji kufikia 2025/26 uwe asilimia 60," alisema.

Alikumbusha kuwa Tanzania ni nchi ya tano kwa uzalishaji wa korofo kati ya 46, takribani mikoa 17 kwa sasa inazalisha zao hilo.

Alisema kuwa mwaka huu wamejipanga kusambaza miche milioni 15 ikiwa ni mkakati wa kufikia tani 700,000 za korosho ghafi ifikapo mwaka 2025/26.



Baadhi ya wakazi wa Mji wa Muheza, wakishuhudia mwili wa dereva wa pikipiki yenye namba za usaji MC 153 CWW Fekon, ukiwa umefunikwa, baada ya ajali ya kugongana na lori la mizigo, eneo la Majengo, barabara kuu ya Segera - Tanga mjini jana. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## Gwajima: Hakuna mtu mdhalilishaji tutakayemvumilia

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, amesema serikali haitavumilia vitendo vya ukatili vinavyoendelea kutokea kwenye jamii.

Waziri Gwajima alitoa angalizo hilo juzi alipotembelea Kata ya Kivule jijini Dar es Salaam kumwona mtoto mwenye umri wa miaka minne aliyefanyiwa ukatili na baba yake mzazi kwa kuunguzwa kwa maji ya moto mkononi kwa kosa la kula mboga bila idhini yake.

"Hatuwezi kuendelea kuvumilia kuona wazazi ambao badala ya kuwa viongozi wanawafanyia ukatili hawa watoto, serikali itamfikia kila mzazi, mlezi na mwanajamii aliyefanya ukatili kwa mwanajamii mwingine hususani watoto," alionya.

Ofisa Utawi wa Jamii wa Hospitali ya Wilaya ya Kivule, Irene Shembelu, ambaye ndiye aliyeibua tukio hilo, alisema mtoto huyo alifanyiwa ukatili huo na baba yake baada ya migogoro ya kifamilia.

Alisema mama wa familia hiyo aliondoka baada ya migogoro hiyo na kuwaacha watoto na baba yao.

"Mtoto huyu aliunguzwa kwa maji ya moto na baba yake kwa kosa la kula maharage waliyotegemea kula baada ya baba kurudi, watoto hawa wanajilea wenyewe, baba akitoka asubuhi anarudi usiku," alisema.

# Serikali yatumia bodaboda kampeni ya kukabili Ebola

**Na Mwandishi Wetu,** BUKOBA

KAMPENI ya kutoa elimu ya kujikinga dhidi ya tishio la ugonjwa wa Ebola kwa madereva wa bodaboda na magari maalum ya kutoa matangazo imezinduliwa mkoani Kagera na Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu.

Kampeni hiyo itakayodumu kwa siku 30, itafanywa na nusu ya madereva wa bodaboda wote wa mkoa huo na magari matano yenye matangazo na wataalamu wa afya yatakayosambazwa katika halmashauri zilizoko hatarini ambazo ni Kyerwa, Karagwe, Ng'ara, Misenyi na Bukoba Mjini.

Ummy akizungumza juzi mkoani hapa baada ya kuzindua kampeni hiyo, alisema watatoa elimu kwa viongozi wote wa bodaboda, viongozi wa vitongoji na vijiji kwa lengo la kufikia wananchi wengi hususan wanaoingia na kutoka kupitia mipaka isiyo rasmi.

"Wasafiri wengi wanatumia mipaka isiyo rasmi zaidi ya 1,000 na wengi wanatumia usafiri wa bodaboda kuwasambaza maeneo mbalimbali, hivyo tumewapa elimu ya kujikinga na kuzitambua dalili za awali na kuwaelekeza watoe taarifa katika ofisi zote za serikali zilizo jirani wakiwamo viongozi wa vitongoji na vijiji, waseme ni wapi wamemwacha ili asaidiwe," alisema.

Waziri Ummy aliwatoa hofu kuwa, ugonjwa huo haujaingia nchini bali wawe mabalozi wa kutoa elimu kwa kutumia kazi yao ya bodaboda kwa sababu ikitokea umeingia, hawataendelea na shughuli zao kama ilivyo sasa.

**TAHADHARI MUHIMU**

Kuhusu hali ya ugonjwa huo, alisema utayari wa kukabiliano nao ni mkubwa, wafuatiliaji wa magonjwa wamewekwa katika vituo vya 351 mkoani humo pamoja na kupima wasafiri katika mipaka yote.

Alisema serikali imewekeza nguvu kubwa katika kutoa elimu kuhusu nini kifanyike na wananchi wanaweza kujikinga vipi na dalili zake ni zipi.

"Watu wanapata wasiwasi kuwa Ebola imeingia, hapana! Hatuna mgonjwa wa Ebola, wasiwasi ni akili kwani ugonjwa ukiingia nchini, tutakuwa tumepoteza! Hivyo lazima tuwekeze nguvu katika kuzuia usiingie nchini kuliko tukae hivi alafu uingie ndio tuanze kutafutana," alisisitiza Ummy.

Waziri huyo pia alitaka kampeni hiyo kutumika kutoa elimu ya chanjo ya UVIKO-19 ili kupunguza hatari ya watu kupoteza maisha endapo ugonjwa wa Ebola utaingia nchini.

Kaimu Mkurugenzi Kitengo cha Elimu ya Afya kwa Umma, Dk. Ama Kasangala, alisema madereva hao walipatiwa flash zenye ujumbe maalum, vipeperushi na vizibao vyenye ujumbe wa elimu ya ugonjwa huo.

Alisema pia watasambaza kwenye usafiri wa umma kama daladala na bajaji kwa ajili ya kutumika kuelimisha wananchi ili iwe rahisi kumbaini mgonjwa haraka na kuepuka madhara makubwa.

Aliwataka wananchi kuendelea kupiga simu namba 199 kutoa taarifa ya mtu mwenye dalili au mwenye swali na itapokelewa na watoa huduma 20 hadi 30 waliopo kituo kikuu cha huduma kwa wateja jijini Dar es Salaam.

Dereva wa bodaboda wilayani Bukoba, Kassim Nuru aliahidi kutumia elimu aliyopewa kuchukua tahadhari na kutoa taarifa endapo atabeba abiria mwenye dalili hizo.

Alisema pia atatumia flash yenye maelezo kufikisha ujumbe kwa abiria atakaowabeba kila siku.

HABARI KITAIFA

# Ukaguzi leseni 40,000 madini kurindima nchini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TUME ya Madini imesema mwaka huu inatarajia kufanya tathmini na ukaguzi wa leseni za madini zaidi ya 40,000 zilizopo ili kuzifuta ambazo hazijaendelezwa.

Vilevile, inatarajia kutoa leseni kubwa moja ya uchimbaji wa madini yanayopatikana kandokando ya bahari (Beachsand) mkoani Tanga.

Katibu Mtendaji wa tume hiyo, Yahya Samamba aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa kuhusu utekelezaji wa bajeti na vipaumbele kwa mwaka 2022/23.

Samamba alisema tume haitavumilia mtu ambaye ameshika maeneo bila kuyaendeleza, akitamka: "Mpaka sasa kwenye kanzidata kuna leseni zaidi ya 40,000 za madini mbalimbali, ili kujua ni ngapi zitafutwa, tutafanya tathmini na ukaguzi.

"Ukirudi nyuma kidogo, tumefuta leseni 163, sasa kwa kipaumbele hiki ili kujua leseni ngapi zitafutwa, lazima kwenda kukagua na hatufuti kupitia mfumo wa leseni tulionao ofisini, tunakwenda kufanya ukaguzi, yule ambaye hafanyi kazi, tunaorodhesha na baadaye tunafuta."

Katibu huyo alisema kwa mwaka 2022/23 wanatarajia kukusanya Sh. bilioni 822, kusimamia ipasavyo miradi ya madini, kuimarisha zaidi hali ya usalama, afya na mazingira ya migodi.

Alisema tayari leseni tatu za uchimbaji mkubwa za madini zimetolewa na kwa sasa kuna leseni moja ambayo ipo kwenye hatua za mwisho itatolewa hivi karibuni.

Pia alisema tume imejipanga kusimamia ipasavyo miradi yote ya madini itakayozalisha nishati safi kwa ajili ya utengenezaji wa betri za magari, nishati ya kuendeshea mitambo mikubwa na madini yatakayotumika katika teknolojia kubwa.

"Matumizi ya madini yanayotumika katika teknolojia kubwa kama ndege, roketi, silaha za kisasa yameongezeka. Tume tumejipanga ipasavyo kusimamia miradi yote ya madini ya Nikel, Lithium, Colbat, Graphite, Ree, Niobium, ili taifa linufaike nayo," alisema.

Alibainisha kuwa zaidi ya leseni 828 za madini hayo zimetolewa kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Alisema migodi 92 imefungiwa katika maeneo ya Geita, Kahama na Singida ili kuokoa maisha yao.

Kiongozi huyo alisema tume itaendelea kudhibiti utoroshaji na biashara haramu ya madini kutokana na serikali kuimarisha masoko ili wachimbaji wauze madini yao ambapo hadi sasa kuna masoko ya madini 42 na vituo vidogo vya ununuzi 83.

"Kwa mwaka wa fedha 2021/22 masoko na vituo hivyo vimechangia Sh. bilioni 164.09 kulinganisha Sh. bilioni 145.23 kwa mwaka 2020/21," alisema.

Alibainisha kuwa kiwango cha makusanyo ya maduhuli ya serikali kutoka sekta ya madini kimeongezeka kutoka Sh. bilioni 346.275 mwaka 2018/19 hadi Sh. bilioni 624.61 mwaka 2021/22 sawa na ongezeko la asilimia 44.5.

"Kupitia mikutano na makongamano ya ndani na nje, tume imeendelea kuvutia wawekezaji ambapo hadi kufikia Septemba 2022, tume imefanikiwa kutoa jumla ya leseni 31,971," alisema.

Pia alisema zaidi ya Sh. bilioni 29.8 zimetumika kwa ajili kutoa huduma kwa jamii zinazoizunguka miradi ya madini kwa kipindi cha kati ya mwaka 2019 hadi 2021.

Mkurugenzi wa Idara ya Habari Maelezo na Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa alisema mtazamo wa serikali kwa sasa ni kupanua wigo wa kunufaika na madini kwa kuwa utafiti wa kubaini madini umefanyika kwa asilimia 16.

"Tunataka tufanye utafiti wa kina kujua madini mengi zaidi angalau kufikia asilimia 40 ili serikali ijenge mazingira mazuri na kuzihamasisha sekta binafsi kuchimba madini hayo," alisema.



Mkurugenzi wa Huduma za Uuguzi wa Hospitali ya CCBRT, Emelda Lwena, akimlisha keki mmoja wa watoto aliyefika hospitalini hapo, mkoani Dar es Salaam mwishoni mwa wiki kwa matibabu kama sehemu ya maadhimisho ya kilele cha wiki ya huduma kwa wateja 2022 yenye kaulimbiu ya "Furahia Huduma". **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Matukio 270 ya ukatili yatikisa Katavi miezi 9

**Na Neema Hussein,**

MATUKIO 270 ya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia yameripotiwa katika Mkoa wa Katavi kwa kipindi cha kuanzia Januari hadi Septemba mwaka huu.

Akitoa taarifa za matukio mbalimbali yaliyotokea ndani ya mkoa huo kwa kipindi tajwa, Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Ali Makame alisema jana kuwa kuna ongezeko la matukio 30 ya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia mwaka huu kulinganishwa na kipindi kama hicho mwaka jana.

Alibainisha kuwa mwaka 2021 kuliripotiwa matukio 240 kwa kipindi cha kuanzia Januari hadi Septemba, hivyo kuwa na ongezeko la matukio 30 sawa na asilimia 12.5.

Kamanda Makame alisema wametoa elimu kwa jamii kuhusu utoaji wa taarifa za matukio hayo kwenye vyombo husika, akisisitiza kuwa ndicho kiini cha ongezeko hilo.

Mbali na hilo, Kamanda Makame pia alisema walifanikiwa kupata silaha mbili aina ya bastola yenye namba 00114704 na gobole lisilokuwa na namba pamoja na risasi 14 kwa nyakati tofauti zikiwa zimetelekezwa wilayani Mlele mkoani Katavi.

Alisema hayo ni mafanikio ya kampeni ya salimisha silaha kwa hiyari ambapo maagizo hayo yalitolewa na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa makamanda wote nchini.

Kamanda Makame alisema wanamshikilia mtu mmoja aliyetambulika kwa jina la Gidioni Manishemwe (20), mkazi wa Sibeyi Buyengero, Burundi kwa tuhuma za kukutwa na risasi moja ya silaha aina ya AK 47 bila kuwa na kibali.

Kamanda Makame pia alisema wanawashikilia watu wengine 25 kwa madai ya kukutwa na pombe aina ya gongo lita 234 pamoja na dawa za kulevya kilogramu 3.7 na miche 112 ya mimea aina ya bangi.

## Jafo aonya vikwazo leseni za uwekezaji

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, amewataka watendaji wa serikali wanaochelewesha nyaraka za uwekezaji kuacha kukwamisha juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan kuvutia uwekezaji.

Akifungua Kongamano la Uwekezaji na Biashara Mkoa wa Pwani jana, Dk. Jafo alisema serikali inapambana katika kuboresha mazingira ya uwekezaji kwa kuunganisha maji, barabara na umeme kwenye maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji.

"Rais ameitangaza nchi kila sehemu na nchi imefunguliwa kwa kila sehemu, hivyo asitokee mtendaji akakwamisha hizi juhudi kwa kuchelewesha nyaraka," alionya.

Dk. Jafo pia aliwataka wawekezaji mkoani humo kuhakikisha wanafungua ofisi na kulipa ushuru kwenye mkoa husika.

"Wapo wawekezaji wamewekeza katika Mkoa wa Pwani lakini ushuru wanalipa walipofungulia ofisi zao ambapo ni Dar es Salam, jambo hili linashusha mapato na halmashauri husika kushindwa kufanya maendeleo.

"Wawekezaji fungueni ofisi Pwani ili wilaya ziweze kupata mapato na kufanya maendeleo kutokana na ushuru na kukuza pato la mkoa na taifa kwa ujumla, siyo mwekezaji amewekeza Pwani ofisi ipo Dar es Salaam na analipa ushuru huko utaratibu huo unakosesha mapato," alisema.

Aliishauri Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kushirikiana na mkoa huo kuandaa kongamano la biashara na uwekezaji ambalo litautangaza zaidi ya mkoa na mikoa mingine ipate fursa ya kufika kujifunza.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge alisema mkoa huo una dhamira ya kuwa mfano katika sekta ya uwekezaji na kwamba kongamano hilo limefanyika kwa lengo kupata ufumbuzi wa vikwazo vya uwekezaji na kuongeza wawekezaji.

Alisema kwa sasa mkoa huo una viwanda 1,460, Kati yake vikubwa ni 90, kongani 23 za viwanda.

Alisema kongani ya Sino Tan ya Kwala inatarajia kuwa na viwanda 350.

Mkurugenzi wa Sino Tan Jensen Huang alisema kwa sasa wanaendelea kushawishi wawekezaji kutoka nje ya nchi kujenga viwanda katika kongani hiyo na itakamilika kwa miaka mitano.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Huduma bora kwa wateja isiwe kwa maadhimisho tu

**WIKI** hii kulikuwa na maadhimisho ya Siku ya Huduma kwa Wateja Duniani, kupitia maadhimisho hayo, viongozi na wafanyakazi wa taasisi mbalimbali za serikali, binafsi na za kimataifa, hushiriki kutoa huduma kwa wateja ama katika maeneo yao ya kazi au kwenye maeneo mengine ya huduma ambako hujitolea kufanya shughuli mbalimbali.

Katika maadhimisho hayo, ndiyo nafasi pekee mteja anaweza kumwona kwa urahisi ofisa mtendaji mkuu wa taasisi bila vikwazo. Nje ya maadhimisho ya huduma kwa wateja, kumwona kiongozi mkuu wa taasisi inakuwa sawa na 'ngamia kupenya tundu la sindano' kwani mwenye uhitaji huo anaweza kuulizwa maswali kadhaa mengine yakiwa hayana majibu. Wakati mwingine unaweza kupewa ahadi iliyozoeleka kwamba njoo kesho au andika ujumbe atakapousoma atakupangia tarehe ya kumwona. Hapo pia kuonana inakuwa majaliwa ya Mungu.

Tofauti na mazoea hayo, wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja, ambayo huadhimishwa kila mwaka, katika baadhi ya benki kwa mfano, maofisa watendaji wakuu, wakurugenzi na maofisa waandamizi huonekana madirishani wakitoa huduma mithili ya makarani wa benki. Pia wakuu hao wa taasisi wanapatikana kiurahisi katika maeneo ya umma ambayo hutoa huduma kuadhimisha wiki hiyo.

Kwenye maadhimisho ya mwaka huu, taasisi mbalimbali zilifanya kama ambavyo zimekuwa zikitoa huduma miaka mingine iliyopita lakini kwa kuongeza ubunifu na ufundi zaidi. Baadhi ya taasisi kama benki na kampuni za simu za mkononi, zilijitolea uchangiaji damu salama katika baadhi ya vituo vya kutolea huduma za afya ili kusaidia wahitaji kama vile wajawazito watoto wachanga na waathirika wa ajali mbalimbali. Kwa kufanya hivyo, wameonyesha kujali kwa kuwa tatizo la damu salama kwa miaka kadhaa sasa ni tatizo sugu.

Tunasema hivyo kwa sababu mara kwa mara tumekuwa tukisikia Ofisi ya Taifa ya Mpango wa Damu Salama ambayo imepewa jukumu la kuhakikisha huduma hiyo inapatikana, ikitoa rai kwa Watanzania kujitokeza kuchangia damu salama ili kuokoa maisha ya maelfu ya wananchi wanaohitaji huduma hiyo. Maadhimisho ya wiki ya huduma kwa wateja, ni jukwaa la kuwakumbusha watoa huduma mbalimbali wakiwamo wakuu wa wizara na idara za serikali juu ya umuhimu wa kufanya kazi zao kwa viwango badala ya kufanya kwa mazoea.


Kwa ujumla, maadhimisho haya ni muhimu kwa sababu viongozi huonekana hadharani na pia baadhi ya kero zinazowahusu wananchi kama vile upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa, malalamiko kuhusu ardhi na mafao kwa wastaafu hupatiwa ufumbuzi kwa viongozi wakuu, wakiwamo mawaziri, kutoa majibu yanayohusu masuala hayo.

Pamoja na umuhimu wa maadhimisho hayo, ni vyema ikaeleweka kuwa suala la utoaji wa huduma ni endelevu badala ya kusubiri matukio, wiki au siku maalum kama ilivyokuwa wiki hii. Jambo hilo ni endelevu kwa sababu kero zinazowahusu wananchi ni za kila siku, hivyo zinahitaji ufumbuzi mara moja badala ya kusubiri maadhimisho.

Kumekuwa na malalamiko mbalimbali yakiwamo rushwa na miongoni mwa taasisi zinazolalamikiwa ni polisi, ardhi, afya na mahakama. Je, malalamiko hayo au maswali yanayoibuliwa na wananchi kuhusu taasisi hizo, yanapaswa kusubiri maadhimisho au utatuzi wa kila siku? Ni muhimu kwa taasisi mbalimbali zinazotoa huduma zikabadilika badala ya kusuburi matukio ndipo zisikilize kero na kuzipatia ufumbuzi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Operesheni hii ya kuchapa wazee kwa tuhuma za uchawi inaturudisha nyuma

**HIVI** karibuni kumeripotiwa taarifa ya kufanyika kwa operesheni ya kuwachapa viboko wazee kwa tuhuma za ushirikina katika Kata ya Kasisi Halmashauri ya Wilaya Urambo mkoani Tabora.

Taarifa hiyo iliyoripotiwa kwenye mitandao ya kijamii, inaeleza kuwa operesheni hiyo iliendeshwa na sungusungu chini ya usimamizi wa diwani wa kata hiyo dhidi ya wazee hao wa kike.

Miaka ya nyuma, mtindo huo ulikuwa kama jambo la kawaida, lakini serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ilijitahidi kuhakikisha unakomeshwa, hasa kutokana na kwamba baadhi ya wazee walipoteza maisha yao.

Hiyo ilitokana na baadhi ya watu kujichukulia sheria mkononi kwa kuwaua wakiwatuhumu kwa ushirikina, hali ambayo ilionyesha kuwa jamii bado iko nyuma hasa wakati huu wa karne ya 21 ya sayansi na teknolojia.

Jitihada zilizofanywa na serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwamo watetezi wa haki za binadamu, zilifanikiwa kuzima mtindo huo wa kujichukulia sheria mkononi kwa kuua wazee kwa tuhuma za ushirikina.

Maeneo yaliyokuwa yakiongoza kwa matukio hayo ni mikoa ya Kanda ya Ziwa, lakini kwa tukio la hivi karibuni la operesheni ya kuchapa wazee kwa tuhuma za ushirikina, ni wazi mtindo huo unataka kurejea upya.

Ninadhani hili si jambo la kufumbiwa macho na kila mpenda amani katika nchi hii, kwani licha ya kuwa linatishia maisha ya watu, pia linaitangaza vibaya nchi katika duru za kimataifa, hivyo lingefaa kudhibitiwa.

Mtindo huo wa kutesa watu kwa tuhuma za ushirikina husababishwa na uelewa mdogo miongoni mwa wananchi sambamba na kutojiamini pale wanapopatwa na matatizo mbalimbali kama vile magonjwa.

Kiongozi kama diwani, hapaswi kushiriki katika vitendo hivyo, badala yake anatakiwa kuelekeza wananchi kuepuka kujichukulia sheria mkononi kwa kisingizio cha ushirikina, jambo ambalo si rahisi kulithibitisha.

Si rahisi kulithibitisha, kwa sababu hiyo ni nadharia tu miongoni mwa watu wanaoamini katika hilo. Hivyo angekuwa mstari wa mbele kuhakikisha jamii anayoiongoza inaelimika na kuachana na mtindo huo.

Kuwapo kwa operesheni hiyo, ni wazi huo ni mwendelezo wa ukatili dhidi ya wazee chini ya mwamvuli wa ushirikina. Vitendo hivyo kama havitadhibitiwa, vinaweza kurejesha mauaji yanayotokana na imani za ushirikina.

Kwa mtazamo wangu, ni vyema wazee wasiwekwe katika taharuki, hali ambayo inaweza kusababisha waishi kwa hofu na kushindwa kutimiza majukumu yao ya kila siku, lakini pia kushindwa kufurahia haki yao ya kuishi.

Waliotuhumiwa kwa ushirikina huko Urambo mkoani Tabora, wamekaririwa na mitandao ya jamii wakiomba serikali kuingilia kati sakata hilo, huku wakilaani kitendo cha wao kuchapwa viboko na vijana wa sungusungu.

Ingependeza kama vyombo vya dola vitafanya uchunguzi kubaini chanzo cha tukio hilo na kuangalia hatua sahihi za kuchukua dhidi ya wahusika wa operesheni hiyo ambayo ni kama inataka 'kufukua makaburi'.

Ikumbukwe kuwa sasa ni miaka kadhaa imepita tangu kudhibitiwa kwa mauaji yanayotokana na imani za kishirikina, lakini operesheni hiyo ya kuchapa wazee, inawezaa kuwa kiashiria cha kurejea mauaji dhidi yao.

Lakini pia ni vyema viongozi wanapofanya operesheni yoyote kuzingatia taratibu ikiwamo kushirikisha jeshi la polisi ambalo kimsingi ndilo lenye dhamana ya ulinzi na usalama ndani ya jamii.

Ukweli ni kwamba, imani za kishirikina zinaweza kuchochea mauaji, ukatili dhidi ya wazee, ikiwamo kubaguliwa au kutengwa na jamii kwa mambo ambayo asili yake ni dhana tu isiyoweza kuthibitishwa.

Kwanini watu wajichukulie sheria mkononi wakati mamlaka zenye dhamana ya kusimamia ustawi wa jamii zipo? Ninadhani tukio hilo la kuchapwa wazee lingekuwa fundisho kwa wahusika kuchukuliwa hatua za kisheria, ili lisijirudie.

## SAFU

### FIKRA MBADALA

# Tunamuenzi Mwalimu kwa matendo?



**Pascal Mayalla**

KARIBUNI tena kwenye safu ya "Kwa Maslahi ya Taifa", yenye mfululizo wa makala zinazozungumzia mada mbalimbali kuhusu taifa letu, ziwe ni za kisiasa, kiuchumi au za kijamii.

Lengo katika safu hii tunaangazia kuhusu kumuenzi Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, mwaka huu atatimiza miaka 23 tangu alipofariki dunia Oktoba 14, 1999 katika Hospitali ya Mtakatifu Thomas, London nchini Uingereza. Kwa kuwa Oktoba 14 ni siku mahususi ya kumuenzi kiongozi huyo na mwasisi wa taifa la Tanganyika na baadaye Tanzania, ni vyema tukatafakari je, Watanzania tunamuenzi Baba wa Taifa kwa mawazo, maneno na matendo?

Mwalimu Nyerere si tu alikuwa ni mwasisi wa taifa bali pia mwasisi wa TANU na baadaye Chama Cha Mapinduzi (CCM). Mpaka kifo chake aliiamini CCM, hivyo hata baada ya nchi Tanzania kuingia kwenye mfumo wa vyama vingi vya siasa mwaka 1992, bado aliamini kuwa wapinzani watatoka CCM.

Nyerere pia aliamini kuwa CCM inaweza kuleta wabunge bora na hili tumelishuhudia kwa baadhi ya wabunge wa upinzani. Walikuwa wabunge bora kabisa lakini kwenye urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mwalimu Nyerere aliamini "Rais bora atatoka CCM pekee." Je, kuna wana CCM wanaomuishi Baba wa Taifa kwa mawazo, maneno na matendo?

**NILIVYOMJUA NYERERE**

Mimi nimezaliwa mwishoni mwa miaka ya 1960, hivyo nimepata akili za kujitambua nilipoanza darasa la kwanza, mwaka 1975 Shule ya Msingi ya Nyakahoja jijini Mwanza, kwa kumsikia tu Rais Nyerere na kumwona kwenye magazeti baba yangu Mzee Mayalla (RIP) akisoma.

Mwaka 1976, baba alipatwa na matatizo kazini, tukahamishwa usiku usiku na landrover 109 za polisi na kupelekwa kijijini Itonjanda huko Tabora. Huku ni kwa bibi mzaa baba, babu mzee wa Kusukuma baada ya kuoa mwanamke wa Kinyamwezi, Mwanza tuliishia kuisikia tu, akahamia jumla Tabora.

Ile mwaka 1977 wakati CCM inazaliwa, nilikuwa darasa la tatu Shule ya Msingi ya Itonjanda. Siku hiyo shule tulichinja ng'ombe na ndiyo mara yangu ya kwanza kushuhudia wanafunzi wanavyogombea nyama. Nikawa nawashangaa maana mimi nilikuwa sipendi nyama ya ng'ombe, nilipenda kuku. Lakini baada ya kufika kijijini, wale kuku waliishia Mwanza.

Mwaka 1978 nikafuatwa kijijini na baba yangu mdogo, Mzee Mathew Kasanga na kwenda kuishi na familia yake jijini Dar es Salaam, eneo la Drive Inn, kanisa letu ni St. Peter, hivyo siku ya kwanza napelekwa kanisani, mimi si mgeni wa kanisa hilo. Tulipoingia, nikashangaa wenzangu wanajazana viti vya nyuma, wakati pale mbele kuna safu za viti vitatu ziko tupu, hivyo mimi na ushamba wangu, nikajiona mjanja ngoja niwahi kukaa siti za mbele, hivyo nikaenda kukaa siti ya kwanza kabisa niko peke yangu!.

Nikaona kama watu wananishangaa shangaa, mara nikafuatwa na mzee mmoja amevaa Kaunda Suti nyeusi na kuniuliza wewe ni nani? Nikamtajia jina, akaniuliza unakaa wapi, nikamjibu. Akaniuliza, wewe ni mgeni kanisa hili, hujui hizi siti za nani? Nikajibu mimi ni mgeni na leo ndiyo mara yangu ya kwanza kuja kanisani. Niliambiwa nimfuate nikatolewa nje huku kanisa zima wanashangaa!. Kule nje nikaitiwa polisi nikabidhiwe nikahojiwe! Ndipo ndugu zangu wakawafuata wale wazee na kuwasihi nisamehewe, nikasamehewa na kurudi ndani.

Baada ya kurudi kanisani, ndipo nikamuona babu mmoja ana nywele nyeusi na nyeupe, ndipo nikamkumbuka ni Nyerere. Akaenda kukaa kwenye benchi zima la pili peke yake! Benchi la kwanza liko tupu na benchi la mwisho wamekaa watu wawili mwanzo wa benchi na mwisho wa benchi! Sasa ndipo nikaelewa kwa nini watu walinishangaa! Hivyo, mimi mwenzenu Nyerere nimemwona 'live' toka mwaka 1978.

Wakati wa kutoka nikaona watu wanatoka kanisani haraka na kupanga foleni pale nje kwenye ngazi kumsubiri Nyerere atoke. Alipotoka akawa anawasalimia watu kwa kuwashika mkono. Jumapili iliyofuata na mimi nikafoleni ila mkono sikushikwa na iliyofuata na iliyofuata, hatimaye nikaacha kufoleni kwa kujua Nyerere hashiki mikono ya watoto.

Baadaye, nikawa mtumishi wa kanisa, nikawa naomba kupangiwa misa ya kwanza, hivyo nikawa namhudumia Mwalimu Nyerere kwa kumshikia kisahani cha hostia na ndipo pia nikayaona meno yake kwa karibu na kuijua maana ya jina la Mchonga.

Tangu hapo nikawa namfuatilia sana. Ile hotuba yake ya kutangaza vita, nikaikariri baadhi ya vifungu na kumuiga, "Uwezo wa kumpiga tunao, sababu ya kumpiga tunayo, nia ya kumpiga tunayo. Tutampiga Amini".

Mwaka 1979 kwenye mapokezi ya mashujaa wetu pale Uwanja wa Taifa (sasa Uwanja wa Uhuru) nilikuwapo na kumshuhudia Mwalimu machozi yakimtoka kutokana na tukio lile.

Baada ya kumaliza shule ya msingi, familia ya Mzee Kasanga ikahamia Mikocheni mkabala na Msasani kwa Nyerere, mimi nikajiunga sekondari ya Tambaza, tulikuwa darasa moja na mmoja wa watoto wa Nyerere akiishi hapo Msasani sasa kwa Nyerere tukawa tunakwenda kucheza.

Baada ya Tambaza nikaenda Ilboru, nikapelekwa nyumbani kwa Makongoro, na Rasta mmoja akitwa Gipsi, tukatokea kupatana na Mako, maana ndege wafananao huruka pamoja!.

Baada ya sekondari nikajiunga na chuo cha Uandishi wa Habari TSJ, ndipo Jumapili moja asubuhi, nikaja kuamshwa na mlinzi wa hosteli, kuwa nina mgeni!, si unajua tena mambo ya ujana, na hosteli, ukisikia tuu una ugeni basi unajua ni ugeni wa type gani, ila asubuhi, tena Jumapili, asubuhi ni hatari!, kunaweza kutokea ajali!.

Kufika nikakuta jamaa fulani mweupe ana bonge la afro na gari sports car nyekundu na kujitambulisha Mimi ni Madaraka Nyerere, mtoto wa Nyerere, unahitajika Msasani kwa Nyerere.

Naomba niishie hapa, tukutane wiki ijayo mjue niliitiwa nini Msasani kwa Nyerere?

**Wasalaam**

**Paskali: Mob. +255 754 270403**

### MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Wateule msaidieni Rais si kila kitu afanye



**Na Joseph Kulangwa**

JUMAPILI iliyopita, Oktoba 2, gazeti hili katika ukurasa wake wa nne, lilikuwa na habari iliyobeba kichwa 'Atinga Ikulu kudai kiwanja chake kilichouzwa miaka 25 (iliyopita)'.

Habari hiyo inamzungumzia mkazi wa kijiji cha Unyabwa mkoani Singida, Asha Ibrahim, mwenye umri wa miaka 53, aliyetinga Ikulu ya Chamwino, Dodoma akiwa na shauku ya kuonana na Rais Samia Suluhu Hassan amsaidie tatizo lake.

Asha aliyekuwa anamiliki kiwanja namba 217 Kitalu B, kiliuzwa mwaka 1997 kwa muuguzi licha ya kukimiliki kwa miaka minne na miaka yote hiyo akikilipia kodi bila kukosa.

Lakini wakati anajiandaa kuanza kujenga akiwa amepeleka saiti mchanga, kokoto na mawe, kirahisi tu akaambiwa na maofisa ardhi kuwa kiwanja hicho si chake tena bali ni cha muuguzi na kumwahidi kupata kingine muda si mrefu.

Kunguru mwoga huyo akakunja mbawa zake na kuzikunjua na kuruka kurudi nyumbani kwake, kusubiri mbadala wa kiwanja chake. Kumbe kwa wale maofisa ndiyo ilikuwa imekwisha hiyo, wakijua hatakuwa na pa kwenda. Na kweli!

Alipoona jua linazama, huku awamu hiyo ya Benjamin Mkapa ikipita kimya, ya Jakaya Kikwete nayo kimyaa, ndipo katika awamu ya John Magufuli akadhani atafanikiwa. Akajitokeza Juni 2019 na kuibukia Manispaa ya Singida kudai. Akaambulia patupu, akaenda mkoani yale yale. Akarudi nyumbani kujilalia akimwachia Mungu.

Magufuli alipoaga dunia, akampa Rais Samia muda kidogo azoee kwenye uongozi wa juu wa nchi, hatimaye akaibuka tena Aprili 4, mwaka huu. Hapo alishauona mwelekeo wa Rais Samia kuwa ni wa kusaidia wanyonge kivitendo.

Huyo, akakanyaga mpaka Chamwino kuonana na Mama. Kufika Ikulu akidhani ingekuwa rahisi kumwona Rais, akaangukia mikononi mwa wasaidizi wa Rais ambao alhamdulilahi walimsikiliza A to Z. Wakamwelewa wakabaini ukweli na haki iliko.

Wakaona iko ndani ya uwezo wao, wakatoa maagizo kwa viongozi wa mkoa wa Singida kushughulikia tatizo lake. Septemba 30, Ijumaa, Asha akapewa hati ya kiwanja kingine na Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba. Asha amefuatilia kiwanja chake kwa robo karne, huku katikati akipata dhoruba ya ajali na kuumia mguu na sasa kuwa na ulemavu. Si hivyo tu, akapata dhoruba ya kiuchumi na sasa hana hata uwezo wa kujenga.

Shukuru Mungu, Serukamba akaagiza Manispaa kumpelekea saiti mpya mchanga, kokoto na mawe aliyokuwa ameshapeleka kwenye saiti aliyonyang'anywa, lakini je atajenga na nini? Uchumi wa mwaka 1997 na wa leo ni tofauti. Pengine serikali pamoja na yote mema iliyomfanyia imsaidie kujenga angalau naye jasho lake likauke.

Lakini sakata hili linatufunza nini? Hatuna viongozi makini katika mifumo yetu. Tuna viongozi wanaosubiri kila kitu afanye au aseme Rais ndipo hatua zichukuliwe! Inakuwaje miaka 25 Mtanzania analia nchini mwake kudhulumiwa kiwanja, viongozi wapo lakini hawafanyi kitu?

Nini kiliwashinda viongozi wa Manispaa ya Singida ambacho wasaidizi wa Rais imewachukua robo karne kuchukua hatua? Asha alikuwa na dhambi gani mpaka anyang'anywe kiwanja na kupewa 'Mtukufu' muuguzi?

Haya ni maswali ambayo Mtanzania wa kawaida anayehisi jinsi Asha alivyoteseka kufuatilia haki yake, anajiuliza. Haiwezekani Watanzania hawahudumiwi waliko mpaka waende Ikulu ndipo wapate ufumbuzi, kuna sababu gani ya kuwa na wawakilishi wa Rais wilayani na mikoani?

Bila shaka wasaidizi wa Rais walikuwa na mambo mengine ya kuhudumia Watanzania, hivyo suala la Asha lisingewahangaisha na kuacha mambo mengi tena mazito ya kitaifa yakilala.

Huu ni ugonjwa uliokithiri katika taifa hili. Tumekuwa tukisikia hata katika kauli za viongozi, wakimsingizia mambo mengi Rais Samia kuwa hilo limesemwa naye, hivyo ndiyo anavyotaka na mengine mengi. Ili likiwa jema wafurahi kwa pamoja, likidoda wamwangushie yeye!

Hiyo pia inaturejesha kule ambako baadhi ya viongozi walikuwa wakitenda uhalifu na uharamia na kusingizia kuwa ni maagizo kutoka juu, kumbe ni matakwa binafsi na kumchafua kiongozi na serikali yake.

Ina maana wasingekuwa wasaidizi wa Rais kumsaidia, Asha asingepata kiwanja, lakini pia hata Serukamba ambaye ni mpya mkoani humo, alipaswa kulijua hilo mapema na kuchukua hatua, kabla Asha hajakanyaga Ikulu kwa suala lililokuwa chini ya uwezo wa Manispaa achilia mbali mkoa.

Tatizo kuu ni baadhi ya viongozi tulionao kutojiamini kuwa wanaweza kufanya mambo yakawa mazuri kwa maslahi ya wananchi, badala yake wanaishi kifadhila wakiogopa kukosea wakatumbuliwa. Usipojiamini katika utendaji, lazima utaharibu tu. Rais Samia ana mzigo mkubwa kichwani tumpunguzie. Alamsiki!

**kulangwasos@gmail.com**

# Makonda afikishwa mahakamani tena

**Na Mwandishi Wetu**

MFANYABIASHARA Patrick Kamwelwe anayeishi jijini New York, Marekani, amefungua kesi ya madai dhidi ya aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, akidai amlipe fidia ya Sh. milioni 247.2.

Hivi karibuni, Makonda alishtakiwa na Mbunge wa zamani wa Ubungo, Saed Kubenea, shauri lililowajumuisha pia Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI) na Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kwa madai ya kushindwa kuchukua hatua za kisheria dhidi ya kiongozi huyo.

Kesi hiyo mpya ya madai namba 234/2022 ilifunguliwa na Kamwelwe mwishoni mwa mwezi Septemba mwaka huu na kupangwa kutajwa Oktoba 13, mwaka huu mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu wa mahakama hiyo, Richard Kabate.

Mbali na Makonda ambaye ni mdaiwa wa pili, mdaiwa wa kwanza katika shauri hilo ni William Malecela, maarufu Le Mutuz.

Katika kesi hiyo, Kamwelwe anaiomba mahakama imuamuru Makonda na mwenzake kumlipa kiasi hicho cha fedha kama fidia anayodai kuwa imetokana na hatua ya wadaiwa hao kuchukua gari lake aina ya Toyota Rand Rover/Range Rover Ronge Sport.

Kamwelwe, maarufu PCK, anadai Makonda ameendelea kuitumia gari hiyo hata baada ya kuondolewa madarakani licha ya kwamba si mali yake halali.

Makonda alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam wakati wa serikali ya awamu ya tano na aliachia cheo hicho kabla ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, akiwa ni miongoni mwa makada wa Chama Cha Mapinduzi waliojitosa kuwania ubunge wa Jimbo la Kigambano, wakiangushwa na Dk. Faustine Ndugulile.

Makonda pia alikuwa miongoni mwa walioshiriki katika mchakato wa kupata Katiba Mpya na baadaye aliteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni kabla ya kuteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa na Rais John Magufuli.

Katika uongozi wake mkoani Dar es Salaam, Makonda alipiga vita ya vitendo vya ushoga na ukahaba pamoja na dawa za kulevya katika mkoa huo wa kibiashara.

Mnamo Januari 2020, Marekani ilitangaza kwamba Makonda na wanafamilia yake watapigwa marufuku kuingia Marekani kwa tuhuma ya kukandamiza haki za binadamu.



Kaimu Mkurugenzi wa Kinga, Elimu ya Afya kwa Umma wa Wizara ya Afya, Dk. Amma Kasangala, akikabidhi vipeperushi vyenye ujumbe wa kuelimisha wananchi kuhusu tishio la ugonjwa wa Ebola, kwa mmoja wa waganga wa kienyeji katika soko la Bunazi, wilayani Misenyi, mkoani Kagera jana. **PICHA: MARY GEOFREY**

## Wakaidi tahadhari Ebola kufungiwa biashara zao

**Na Mary Geofrey,**
BUKOBA

SERIKALI imesema itafunga biashara za wafanyabiashara ambao watakaidi kuweka vifaa vya kujikinga na tishio la ugonjwa wa Ebola katika mpaka wa Mutukula wilayani Misenyi mkoani Kagera.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Misenyi, Dk. Daniel Chochote, alitoa angalizo hilo juzi wilayani mwake wakati wa ziara ya kukagua utayari wa wafanyabiashara katika kujikinga na tishio la Ebola.

Dk. Chochote alisema tayari wametoa elimu ya kutosha na tahadhari wanazotakiwa kuzichukua ili kuepuka kupata maambukizi ya ugojwa huo.

"Kuanzia leo (juzi), wafanyabaishara wote watakaokaidi kuweka vifaa vya kunawia mikono nje ya maduka yao, wanasema hiari inashinda utumwa, tukifikia hapo tutalazimika kuwafungia maana bora kubaki na wafanyabiashara wachache ambao watahakikisha Ebola haiingii nchini," Dk. Chocholo alionya. Alisema wamewataka wananchi wanaoingia na kutoka kuzingatia kanuni za afya ili ugonjwa huo usiingie nchini.

Diwani wa Mtukula, Swalehe Chakula alisema wameshatoa elimu kwa wananchi na wafanyabiashara na kazi inayoendelea ni kuhimiza waweke vifaa vya kunawa mikono nje ya biashara zao.

Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kinga, Kitengo cha Elimu ya Afya kwa Umma, Dk. Ama Kasangala, alipongeza juhudi zinazofanywa na serikali kuzuia ugonjwa huo usiingie nchini.

Dk. Kasangala aliahidi kuendelea kutoa elimu, kuweka mabango na vipeperusi pamoja na watumishi wa afya waliopo mipakani kuwapima wanaongia na kutoka nchini ili kuzuia ugonjwa huo.

## Mhagama ataka utatuzi wa haraka kero za watumishi

**Na Halfani Chusi**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, amewataka wajumbe wa mkutano wa tatu wa baraza kuu la nne la wafanyakazi Tanzania Bara kuhakikisha wanashughulikia kwa wakati malalamiko ya watumishi wa umma na wananchi katika maeneo yao ya kazi.

Alitoa maagizo hayo juzi mjini Morogoro alipofungua mkutano huo, akisisitiza hakuna haja watumishi kulazimika kusafiri hadi makao makuu ya nchi mkoani Dodoma kutafuta ufumbuzi wa masuala yao ya kiutumishi.

"Wajumbe wa baraza mnaposhughulikia malalamiko ya watumishi na wananchi, mhakikishe mnayashughulikia kwa wakati ili kuwaondolea mzigo wa gharama katika kutafuta ufumbuzi kwa viongozi na waajiri kwenye ngazi ya kitaifa. "Serikali imekuwa ikisisitiza umuhimu wa watendaji kushughulikia malalamiko ya watumishi wa umma ili kuwajengea ari na morali ya kutoa huduma bora kwa wananchi," alisema.

Waziri huyo alisema wajumbe wa baraza hawana budi kuunga mkono jitihada hizo na kuhimiza ushughulikiaji wa malalamiko ya watumishi wa umma na wananchi ambao ndiyo walengwa wakuu wa huduma zinazotolewa na taasisi za umma nchini.

Pia alitoa wito kwa waajiri kutumia mfumo wa e-Mrejesho katika kushughulikia malalamiko ili kupata mrejesho utakaotumiwa na serikali kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Makamu Mwenyekiti wa Baraza Kuu la Wafanyakazi katika Utumishi wa Umma, Jane Mihanji alisema baraza hilo litatoa kipaumbele cha matumizi ya e-Mrejesho serikalini, ili kuendana na kasi ya matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ambayo inakua kwa kasi kubwa.

# MAISHA

OKTOBA 9, 2022
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili



Ukurasa 13


**Mwendo wa ndala**



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Mambo ya kuzingatia unapotafuta eneo la kujenga nyumba



Ukurasa 12

**HARUSI**




# Manukato na urembo

Ukurasa 14

# WATOTO


MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | K | W | E | T | U |
| ■ | W | ■ | ■ | W | ■ |
| B | E | I | ■ | A | ■ |
| ■ | N | ■ | A | N | A |
| ■ | Y | ■ | ■ | G | ■ |
| T | E | N | G | A | ■ |


## AMSHA AKILI




## TOA TOFAUTI 5



## PAKA RANGI




## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
LIA, TOA, TAMBO, SHAKA,
KOKOTO, SHINDA

## CHEKA



Alichokifanya Adaktari

MTOTO John alikuwa akimsaidia baba yake kuchunga mbuzi katika pori la jirani ya nyumba yao. Walipokuwa wakiendelea kuchunga John alimfuata baba yake na kuanza kumuuliza.

**John:** Baba eti mwalimu kasema kweli kwamba fimbo ya mbali haiuwi nyoka?

**Baba:** Ndio mwanangu

**John:** Kwa hiyo ukitaka kuua nyoka uwe na fimbo karibu kama hawa mbuzi?

**Baba:** Kweli mwanangu, lakini mwalimu wako alikupa msemo huo akimaanisha kwamba kilicho karibu yako ndicho kinakusaidia wakati wa shida.

**SWALI**

Taja faida ya zao la mkonge.

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Amdharau mama yake mzazi, kisa amefanikiwa kuwa daktari!

***KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na simulizi ya dada aliyemdharau mamaye, kisa amefanikiwa. Alisahau mahangaiko ya mama yake hata kufikia cheo cha udaktari. Je, ataishia maisha ya aina gani?.***

Wiki iliyopita nilieleza jinsi mama alivyopambana kwa kufanya kazi mbalimbali kama kufua nguo za watu, kuuza mbogamboga ili mradi ale na kumsomesha binti yake. Alijitahidi hata akamaliza darasa la saba na akabahatika kupata wafadhili wakamwendeleza hadi chuo kikuu. Akafaulu vizuri na kupata kazi ya udaktari. Kumbuka nilieleza kuwa hakuwa na baba alifariki, hivyo kuwa mwana pekee kwa mama yake.

Mama hakutaka kuolewa tena akaelekeza nguvu kumtunza binti yake. Lakini cha ajabu, hata baada ya kupata kazi hakumkumbuka tena mama yake. Mama akawa anadhani pengine binti yake hayupo hai kwani ilipita miaka 14 bila kujua habari zake.

Binti akawa na marafiki zake huko mjini na fedha zake akawa anafurahia nao hakumtaka tena mama yake. Akapewa nyumba nzuri na walinzi kumlinda pamoja na gari kwani alikuwa daktari mkubwa. Akawa anawaambia rafiki zake kuwa hana baba wala mama wala ndugu. Kumbe mama yupo hai anaishi bado maisha duni!

Hebu leo msomaji wangu tuone nini kiliendelea kwa binti huyu daktari. Siku moja dada huyu akakutana na kijana ambaye walisoma wote shule kule kijijini. Wakafurahi sana kuonana kwani ilishapita miaka 14 tangu waonane.

Dada akamwambia nipo hapa kwenye hospitali, nina cheo cha udaktari na nyumbani kwangu ni pale. Wakaongozana hadi nyumbani kwake, kijana akafurahia mafanikio yake! Wakakumbushana ya shule, wakacheka kisha kijana akaondoka zake.

Ikapita takriban miaka miwili hivi kijana akaenda kijijini kutembelea jamaa zake. Akiwa huko akakutana na mama yake yule dada daktari. Akamshangaa, Jamani mama upo? Mama alikuwa bado katika hali duni kama alivyomwacha zamani.

Yaani hakuna kilichobadilika kwake. Kijana alilia sana akijiuliza inakuwaje nimekutana na binti yake maisha mazuri ya kifahari. Kwa nini mama anaishi maisha mazingira magumu?

Hali hiyo ilimsumbua sana, akamwambia, mama, nilikutana na binti yako. Mama akasema hapana , umekosea, huenda uliona vibaya. Akamwambia, hapana, tumepiga hadi picha kwa simu hii, huyu hapa muone!(akamwonyesha).

Mama anaangalia picha ya mtoto wake, anaona ni kweli ndiye, kawa mdada kapendeza. Akamwambia kwa sasa ni daktari mkubwa kule jijini Dar es Salaam. Mama aliwaza mengi akijiuliza nini kimemfunga binti amsahau wakati wako wao wawili tu?

Mama akamwambia kijana, kwa sababu umesema utarudi mjini Ijumaa, basi ngoja nijiandae twende wote nikamwone kwa macho. Kijana akasema sawa kwa kuwa najua hadi nyumbani kwake tutakwenda kwa neema ya Mungu!

Ijumaa ikawadia wakaondoka hadi nyumbani kwa binti yake. Wakakuta bado hajarudi toka kazini. Walikuwapo walinzi, kijana akawakabidhi na kuwaambia kuwa huyu ni mama mzazi wa daktari. Wakabaki wanashangaa kwa kuwa dokta alishasema hana baba wala mama wala ndugu yoyote.

Baada ya saa kadhaa daktari akafika nyumbani walinzi wakamwambia, bosi kuna mgeni wako. Akamwangalia kwa dharau, mama akafurahi akanyanyuka amsalimie. Binti akarudi nyuma akamwambia 'do not touch me! '(usiniguse)!

Mama Kiingereza hajui, akadhani amemwambia karibu, kumbe amemnyanyapaa. Mama anazidi kumkaribia, binti anamwambia, usiniguse, umepotea njia? Mama akashtuka, kumbe ndiyo maneno yako hayo ya kimombo yalikuwa yakimaanisha? Nilidhani unanikaribisha mwanangu kumbe unanifukuza?

Mama akamtaja bintiye kwa majina yake. Akamuuliza nini kimekupata? Nani kakuroga? Naye akamjibu; mimi sina baba wala baba. Mama akamwambia, yaani ulishanizika? Mama alifadhaika sana, akaishiwa nguvu akatafuta sehemu akakaa chini.

Yule dada akaingia zake ndani kwa jeuri bila kujali na kuendelea na shughuli zake. Mama akaanza kuwaza jinsi alivyokuwa anahangaika kukata kuni na kuuza, kufua nguo za watu na kutembeza biashara ya mboga mboga ili aweze kupata mlo wa siku pia kumsomesha binti yake huyu.

Lakini leo amefanikiwa ananiambia usiniguse, tena kwa kimombo ambacho mimi sikusoma, naye anajua hilo? Mama akajitia nguvu kwa Bwana na kumuomba Mungu amsamehe asije akatamka mabaya kwa binti yake.

***Mpenzi msomaji, kisa kinaendelea Jumapili ijayo. Je, mama alienda wapi usiku ule? Je, una kisa? Ujumbe 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Utungaji sheria za ukatili uwe shirikishi kufikia suluhisho kudhibiti matukio hayo

MWISHONI mwa wiki kulikuwa na Tamasha la Jinsia, Kanda ya Kaskazini lililoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), likiwa na kaulimbiu 'Haki Endelevu za Uchumi: Rasilimali Ziwanufaishe Wananchi Walioko Pembezoni kwa Maisha Endelevu'. Kongamano hilo liliwakusanya zaidi ya wanaharakati 600 kutoka maeneo mbalimbali ya Tanzania Bara.

TGNP kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wanaotetea haki za wanawake na usawa wa kijinsia, wanaharakati binafsi na kwa ufadhili wa Ubalozi wa Canada, Sweden, Coady Institute Canada, Seedchange, waliandaa tukio hilo muhimu ambalo pia limeoyesha fursa za kiuchumi kwa wanawake na jamii kwa ujumla.

Tamasha hilo lilitumika kama jukwaa la wazi kwa ajili ya wanawake na wadau wa haki za binadamu ambao hukutana pamoja kila baada ya mwaka mmoja kubadilishana uzoefu, kusherehekea, kutathmini na kupanga mipango ya kukabiliana na changamoto zinazowakabili.

Aidha, kongamano lilitoa fursa ya kutafakari na kutathmini changamoto zilizopo na namna ya kuweka mikakati ya kukabiliana na changamoto hizo, haki za uchumi wezeshi, fursa za kilimo kuyanufaisha makundi yaliyo pembezoni kwa maisha endelevu.

Nyingine ni uongozi shirikishi, chachu ya haki za kiuchumi na maendeleo endelevu, mila kandamizi kikwazo cha haki za uchumi kwa maendeleo endelevu boresha upatikanaji wa huduma za jamii, ili kuwezesha upatikanaji wa huduma za afya ya uzazi kwa wote, harakati za ujenzi wa nguvu za pamoja na msingi wa maendeleo jumuishi na endelevu kwa wote.

Hadi mwisho wa tamasha hilo, ilionekana kwamba ukatili wa kijinsia bado ni tatizo kubwa linalorudisha nyuma maendeleo ya watoto wa kike na wanawake, huku mabadiliko ya tabia nchi yakiwa ni tishio jipya la ukatili dhidi ya kundi hilo linalojikwamua.

Aidha, washiriki walieleza namna gani kwa sasa kuna shida ya maji, chakula na malisho ambayo ndiyo kazi ya wanawake ambao wengi wanatembea umbali mrefu kutafuta mahitaji muhimu huko kutokana na hali ya umaskini. Watoto wa kike wanaacha shule ili kusaidia familia zao.

Washiriki waliona kwamba mabadiliko ya tabianchi ni suala la dunia na haliishi leo au kesho bali ni lazima kuwa na mikakati ya kuishi nalo ikiwamo kubadili aina ya mazao wanayolima, mbegu zinazohimili ukame au za muda mfupi na kuvuna maji ya mvua.

Kikwazo kingine ni umiliki wa ardhi kwamba mwanamke anapoolewa anakosa haki ya umiliki kwa wazazi wake na anapokwenda kwa mume nako anakosa haki, hivyo anabaki njia panda.

Washiriki walieleza wanawake wameishia kuwa wakodishwaji wa ardhi na vibarua kwa kuwa licha ya sheria kuwapa haki lakini bado mila na desturi zimekuwa juu ya sheria.

Aidha, TAMISEMI ilieleza maelekezo yaliyotolewa na serikali kwamba kila halmashauri itunge sheria ndogo za kukabili ukatili wa kijinsia na katika kila kikao cha kuanzia ngazi ya kitongoji au mtaa moja ya agenda iwe ni namna ya kukabili ukatili wa kujinsia kwenye eneo husika.

Akifunga tamasha hilo, Mkuu wa Wilaya ya Same, Edward Mpogolo, alieleza uzoefu wa uongozi kwamba alikutana na madai ya wanafunzi kupewa mimba, mama wa mtoto alisimama kidete kutaka sheria ichukue mkondo wake lakini alizidiwa na mambo ya kimila akaikana kesi iliyokuwa inaendelea.

Mpogolo alisema haitakiwi desturi zikawa juu ya sheria bali sheria iwe juu ya mengine yote, lakini iwapo jamii itatanguliza mila na desturi zao waathirika wakuu ni wanawake na watoto.

Aliahidi kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Same itatunga sheria ndogo za ukatili wa kijinsia na kufuatilia usimamizi wake ili kuhakiksiha zinatekelezwa kuanzia ngazi ya kitongoji katika kufikia agenda ya kitaifa.

Nawaza kwa sauti kwamba ikiwa kila halmashauri itatunga sheria ndogo ambazo zitapita katika mchakato shirikishi kuanzia kitongoji au mtaa, kata hadi wilaya ni wazi kuwa jamii itajua sasa kuna sheria mahususi na yeyote atayeharibu kuna hatua kali dhidi yake.

Kukiwa na ushirikiano baina ya wanaoandaa sheria na wananchi itakuwa jambo jema maana litakwenda kutatua tatizo linalokuwa kwa kasi licha ya jitihada za miaka mingi kupinga ukatili dhidi ya watoto, wanawake na makundi mengine kwenye jamii.

Natambua utaratibu wa kutunga sheria kwamba yanakusanywa maoni, inatengenezwa rasimu ambayo itakwenda kwa wadau (wananchi) kisha watajadili na kutoa maoni zaidi ambayo yatakusanywa na kutengeneza rasmili nyingine itakayokwenda kwenye Baraza la Madiwani kwa mjadala kabla ya kupata nakala halisi ambazo baada ya kupitishwa na baraza na mamlaka za mkoa na wilaya, huridhiwa na waziri mwenye dhamana ya serikali za mitaa na baadaye Bunge.

Ni muhimu sana kwa wakati huu ambao ukatili wa kijinsia umeshamiri sheria hizi zikatungwa kwa ushirikishwaji wa tofauti na sheria nyingine, tuone namna gani eneo dogo la utawala (wilaya) linaweza kutunga sheria nzuri ambayo itakuwa mwarobaini wa ukatili wa kijinsia.

# SIKU YA POSTA DUNIANI 9 OKTOBA, 2022.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI**



MHESHIMIWA NAPE MOSES NNAUYE (MB),
WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI

## UJUMBE KUTOKA KWA MHESHIMIWA NAPE MOSES NNAUYE (MB), WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WAKATI WA MAADHIMISHO YA SIKU YA POSTA DUNIANI TAREHE 9 OKTOBA, 2022

Kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nichukue nafasi hii kueleza kuwa Tanzania inafuraha kuungana na nchi nyingine Duniani katika kuadhimisha Siku ya Posta Duniani kwa mwaka 2022 tangu kuanzishwa kwa Umoja wa Posta Duniani (UPU) mwaka 1874. Mtandao wa Posta duniani umewezesha nchi nyingi ikiwemo Tanzania kunufaika na huduma za mawasiliano kwa kuwafikia wateja wake popote walipo ndani na nje ya nchi.

Maadhimisho hayo yamefika wakati muafaka ambapo Tanzania imetoka kuhitimisha zoezi la Kitaifa la Sensa ya Watu na Makazi ambayo itatoa nafasi kwa Shirika la Posta la Tanzania kuboresha huduma za kiposta kwa urahisi na ustadi zaidi. Sekta ya Posta imekuwa ni moja ya Sekta za kipaumbele chini ya maelekezo ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ameelekeza kuwa utambuzi wa Anwani za Makazi ni muhimu kutokana na mchango wake wa maendeleo kwa huduma za kijamii na biashara kwa Taifa.

Kauli mbiu ya mwaka huu ya **'Posta kwa Kila Mtu' (Post for Planet)** inahamasisha Sekta ya Posta kuzingatia pia mabadiliko ya tabia nchi ambayo yamesababisha mgogoro mkubwa wa hali ya hewa katika Mabara yote Duniani, kuathiri afya na ustawi wa binadamu. Kadhalika, huduma za posta zimesaidia kuunganisha watu na jamii katika mipaka, kuendeleza mtiririko na ubadilishanaji wa taarifa, kuwezesha usafirishaji wa bidhaa na utoaji wa huduma za kifedha na nyinginezo. Hivyo, tunaungana na nchi nyingine ambazo ni washirika wa huduma za posta katika kuhakikisha kuwa huduma hizo zinapunguza athari za mabadiliko ya hali ya hewa na afya ya vizazi vijavyo.

Wizara inapongeza Shirika la Posta Tanzania kwa kutekeleza Sera ya Taifa ya Posta (2003) pamoja na mfumo wa udhibiti wa posta nchini Tanzania. Sekta ya Posta ni kichocheo cha maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa nchi, kwa kuzingatia malengo ya Taifa na mifumo imara ya mawasiliano na uendeshaji wa Sekta ya Posta.

Natoa rai kwa Shirika la Posta Tanzania kuhakikisha inajipangia mikakati madhubuti ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa:

(1) Kupanda miti kwa wingi, kulinda viumbe hai na kupunguza uzalishaji wa kaboni kutoka kwa magari;
(2) Kutokomeza matumizi ya mifuko ya plastiki na badala yake kutumia vifungashio vinavyotunza mazingira.

Tanzania iko tayari kushirikiana na nchi wanachama wa Umoja wa Posta Duniani (UPU) kwa kuzingatia kuwa huduma za kiposta zinaboreshwa ipasavyo kuanzia miundombinu, usafiri na usafirishwaji salama wa bidhaa kwa wateja. Huduma hizo za kiposta zitazingatia utunzaji wa mazingira, mabadiliko ya tabia nchi na kuhakikisha kuwa huduma za kiposta ni salama, rafiki na zinapatikana kokote ulimwenguni.

Nawatakia maadhimisho yenye mafanikio ya Siku ya Posta Duniani 2022.

**ASANTENI**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI**
**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**



**Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dkt. Jabiri K. Bakari**

## UJUMBE WA MKURUGENZI MKUU WA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA (TCRA), DKT. JABIRI KUWE BAKARI WAKATI WA MAADHIMISHO YA SIKU YA POSTA DUNIANI, TAREHE 9 OKTOBA 2022

Tanzania ikiwa ni miongoni mwa nchi wanachama wa Umoja Posta Duniani (UPU) inaungana na nchi nyingine 192 katika kuadhimisha kumbukumbu ya kuanzishwa kwa UPU kwa madhumuni ya kujenga uelewa wa nafasi ya sekta ya posta kwa jamii katika shughuli zao za kila siku na mchango wake katika maendeleo ya kiuchumi.

Kauli mbiu ya Siku ya Posta Duniani kwa mwaka 2022, "Posta kwa Kila Mtu", inalandana na kazi ya kila siku ambayo Posta zimekuwa zinafanya, ambayo ni kuhakikisha dunia inaendelea kuwa ya kijani kwa vizazi vijavyo. Ni muhimu sasa kufikiria upya jinsi tunavyoendesha biashara na kubadilisha mifumo yetu ya matumizi ya nishati ili kupunguza hewa ya ukaa. Katika Dunia yetu inayozunguka, mambo hayatulii kamwe; yanaendelea kusonga mbele na kubadilika na kwa mwendo huo mifumo ya hali ya hewa pia inabadilika; ama vyema au vibaya.

Posta ipo kila mahali kwenye sayari yetu. Posta inaweza kuwafikia walio hata maeneo ya mbali zaidi kwenye sayari yetu ili kutoa huduma mbalimbali kwa kila mtu. Katika kufikisha vifurushi na barua, au huduma za kifedha, huduma za kijamii na afya, au msaada wa kibinadamu, Mashirika ya Posta na washirika wao hutoa huduma kwa kuzingatia uelewa wa wateja kuhusu mazingira.

Siku hizi masuala ya mabadiliko ya tabianchi ni mtambuka na yanagusa maeneo yote ya sera za serikali. Kwa kuzingatia hayo, Umoja wa Posta Duniani ambalo Tanzania ni mwanachama limechagua kauli mbiu "Posta kwa Kila Mtu" ili kuibana sekta ya Posta kuungana na washirika wengine kufanya kazi kwa pamoja katika kuhifadhi mazingira.

Aidha, katika kipindi hiki cha msukosuko wa kiuchumi, usimamizi mzuri wa masuala ya mazingira unaweza kuwa msukumo mkubwa wa maendeleo. Katika kukabiliana na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi, mashirika ya posta yanaweza kufikiria upya michakato ya kilojistiki, kuboresha ufanisi, kupanga hatua za muda mrefu za kuokoa nishati, kuwa wabunifu wa TEHAMA, kuja na bidhaa na huduma mpya ambazo ni rafiki kwa mazingira.

Kwa mtazamo wa kiudhibiti, huduma nyingi za Posta bado zinatekeleza mambo mengi ambayo yanaweza kusababisha uharibifu wa asili na yasipodhibitiwa yataleta athari mbaya kwa mazingira yetu. Sekta ya Posta inatumia vifungashio ambavyo vimetengenezwa kwa malighafi mbalimbali ikiwa ni pamoja na plastiki, pamba, na kitani, kwa kutaja tu baadhi. Sekta pia inatumia motokaa, vifaa vya kielektroniki, magari madogo ya vipeto na vifurushi, ndege na treni kubeba na kufikisha barua kwa wateja. Matumizi ya mifuko ya plastiki ni hatari kwa mazingira na uchafuzi wa hewa na hatari nyingine ya mazingira. Kwa kuzingatia athari za shughuli za posta, sekta imechukua hatua za kuzuia uharibifu kwa mama yetu asili. Ili kusimamia taka za kielektroniki na vifaa vya mawasiliano vya kielektroniki vinavyoingizwa nchini au kutengenezwa kwa ajili ya matumizi ya Jamhuri ya Muungano katika kuunganishwa kwenye mtandao wowote wa mawasiliano ya kielektroniki kwa madhumuni ya kupokea au kusambaza mawimbi ya mawasiliano ya kielektroniki, TCRA imeandaa Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Viwango vya Vifaa vya Mawasiliano vya Kielektoniki na Usimamizi wa Taka za Kielektroniki) za mwaka 2020. TCRA imebuni mfumo wa utoaji leseni rafiki ili kuhakikisha kiwango cha ubora katika huduma za posta kinaboreshwa kwa wateja mbalimbali na tunatarajia kwamba, wateja wa posta wataendelea kunufaika na chaguzi zaidi za huduma za posta zinazoeleweka, za kibunifu na zenye kukubalika.

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kama Mdhibiti wa Sekta na kwa kushirikiana na wadau wengine inatafakari namna ya kukabiliana na hali mbaya ya hewa kwa kufanyia kazi yafuatayo: -

- Kuongeza uwezo wake wa kustahimili mabadiliko ya tabianchi, na kuonesha ushirikiano baina ya wadau wa hali ya hewa.
- Kuwahimiza wadau wa posta kuthamini umuhimu wa kuwa na mazingira safi, na hivyo kuweka bajeti ya kuwezesha nchi kupunguza hewa ya ukaa.

TCRA inapenda kuwahimiza wadau na watendaji wote wa sekta hii kutekeleza kauli mbiu ya mwaka huu. Kwa kuhitimisha ujumbe wangu, napenda kuutaarifu umma kwamba, TCRA hadi kufikia Septemba, 2022 imetoa leseni kwa watoa huduma wa posta 90 katika makundi matano kama ifuatavyo:

| Na. | Aina ya Leseni | Jumla |
|---|---|---|
| 1 | Mtoa Huduma za Posta wa Umma | 1 |
| 2 | Huduma za vipeto na vifurushi kimataifa | 6 |
| 3 | Huduma za vipeto na vifurushi ndani ya nchi | 27 |
| 4 | Huduma za vipeto na vifurushi ndani ya mji mmoja | 13 |
| 5 | Huduma za usafirishaji kati ya miji miwili | 43 |

Mwisho, naomba niwapongeze watoa huduma za posta Tanzania kwa kuwa mstari wa mbele katika kulinda mazingira kwa ajili ya maendeleo bora ya kijamii na kiuchumi ya taifa letu na kutimiza matarajio ya Watanzania.

Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi ya TCRA, Menejimenti na Wafanyakazi nawatakia wadau wetu wote wa posta Heri ya Siku ya Posta Duniani.

UPU UNIVERSAL POSTAL UNION



MKURUGENZI MKUU WA UPU -MASAHIKO METOKI

## UJUMBE WA MKURUGENZI MKUU WA UMOJA WA POSTA DUNIANI (UPU), NDG. MASAHIKO METOKI, SIKU YA POSTA DUNIANI, TAREHE 9 OKTOBA 2022

**Kauli mbiu: "Posta kwa Kila Mtu"**

Hatuwezi tena kupuuza mabadiliko ya ghafla ya hali ya hewa. Mabadiliko makubwa katika mazingira yetu yanaanza kuwa na athari kubwa katika maisha na mistakabali yetu ya kila siku.

Makubaliano ya kisayansi ni bayana: shughuli za kibinadamu zinaleta mabadiliko ya tabianchi. Mashirika ya kimataifa, serikali na asasi za kiraia zimetoa wito kwa sekta zote kuchukua hatua za haraka ili kuepusha athari mbaya zaidi za janga hili.

Sekta ya posta inaajiri zaidi ya watu milioni 5 wanaofanya kazi kwenye ofisi zaidi ya 600,000 katika nchi 192. Inatoa mamia ya mabilioni ya bidhaa za posta kwa mwaka. Bila shaka sekta ya posta na washirika wake wana jukumu la kuchukua hatua madhubuti ili kupunguza hewa ya ukaa wanayozalisha. Lazima tulete mabadiliko ndani ya sekta yetu wenyewe.

Katika kuadhimisha Siku ya Posta Duniani mwaka huu, tumechagua kauli mbiu "Posta kwa Kila Mtu". Kama mshiriki wa kimataifa katika utoaji wa bidhaa na huduma muhimu, Mashirika ya Posta yako katika nafasi nzuri ya kuonyesha njia kwa washirika wao katika mnyororo mzima wa ugavi kimataifa. Wanaweza kuwa mstari wa mbele katika upunguzaji wa athari za hewa ya ukaa, uhimilivu na ustahimilivu ndani ya sekta nyingine.

Kupambana na mabadiliko ya tabianchi sio kazi ndogo. Hatua madhubuti zinahitaji uwekezaji madhubuti, lakini uwekezaji huu utaleta faida kwa siku zijazo.

Hatua juu ya mabadiliko ya tabianchi itasukuma pia mwelekeo wa malengo ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Lazima tufikirie athari zitakazotupata zaidi ya tunavyofikiri juu ya ofisi zetu, mitandao yetu na mipaka yetu. Kila mtu, kampuni na taifa kwenye sayari hii ana jukumu katika vita hii. Ni lazima sote tushirikiane ili kupata mustakabali bora kwa vizazi vijavyo.

Nazisihi serikali za nchi wanachama wa UPU zifanye kazi na washirika wa umma na wa binafsi ili kuwekeza katika hali ya hewa kwa ajili ya sekta ya posta.

Natoa wito kwa Posta kufufua ari ya uvumbuzi ambayo iliwasaidia kuunga mkono jumii zao wakati wote wa janga la UVIKO-19. Tumieni uzoefu huo kupata majawabu ya kibunifu ambayo yatapunguza kiwango cha hewa ya ukaa, na kuwa kigezo cha kutafuta majibu sahihi na yenye tija ili kusaidia jumuiya zenu

Mwisho, nawaomba mabilioni ya watu wanaotumia Posta kila siku kuisaidia sekta yetu tunapofanya kazi ya kujenga mustakabali bora na angavu.

**Nawatakia maadhimisho mema ya Siku ya Posta Duniani.**

Posta Let's Go!

**SHIRIKA LA POSTA TANZANIA**



**POSTAMASTA MKUU, Macrice Daniel Mbodo**

## SIKU YA POSTA DUNIANI

**Kauli mbiu: "Posta kwa Kila Mtu"**
**UJUMBE KUTOKA KWA POSTAMASTA MKUU**

Leo tarehe 9 Oktoba, 2022 Shirika la Posta Tanzania (TPC) linaungana na wadau wa huduma za posta duniani kuadhimisha Siku ya 148 ya Posta Duniani, maadhimisho ya kuanzishwa kwa Umoja wa Posta Duniani (UPU) yalifanyika mwaka 1874.

Kihistoria tangu zamani, aina tofauti za huduma za posta zimekuwa sehemu muhimu ya ustaarabu wa binadamu hadi leo. Kutokana na kihistoria hii, jumuiya ya posta duniani inaadhimisha Siku ya Posta Duniani kwa mwaka huu chini ya kauli mbiu –"Posta kwa Kila Mtu".

Kwa kuzingatia kauli mbiu hii, Shirika la Posta Tanzania kama Mtoa Huduma za Posta kwa Umma katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linafahamu vyema kwamba katika dunia ya sasa yenye kubadilika badilika, mashirika yenye kuendesha biashara na huduma yanapaswa kubadilika na kuendana na mazingira ya kijamii, kiuchumi na kiteknolojia yanayobadilika kwa haraka. Na kwa mantiki hii, TPC inapaswa kujitahidi kufanya lolote linalowezekana kumhudumia kila mwananchi popote alipo.

Kwa njia hiyo, Shirika la Posta Tanzania limeanzisha bidhaa za kidijitali kwa madhumuni hayo hayo ya kuhudumia jamii nzima kwa urahisi. Kimsingi tunajua kwamba mabadiliko ni jambo la kudumu na kwa hiyo Shirika linafahamu vyema kwamba ongezeko la jumla la utoaji wa huduma za kidijitali, Teknolojia za Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ni kipengele muhimu cha kubadilisha na kuchagiza mustakabali wa Sekta ya Posta kwa ngazi zote (za kitaifa na kimataifa). Nia yetu ni kutumia teknolojia hizi mpya katika utoaji wa huduma za mawasiliano za pamoja ili kuwafikia wananchi wote popote walipo.

Tumeanzisha HUDUMA kwa njia ya tovuti inayojulikana kama "POSTA KIGANJANI" ambapo kwa huduma zetu za posta zinaweza kufikiwa na wateja wetu wakati wowote kirahisi kupitia simu za mkononi. Huduma kama vile maombi ya masanduku ya posta, huduma za miliki, huduma za kupokea na kufikisha mali, huduma za kufuatilia na kujua kama bidhaa za posta zimesajiliwa, vifurushi au barua za haraka zinaweza kupatikana kirahisi. Kwa hiyo, kila raia sehemu yoyote alipo anaweza kupata huduma zetu. Hivyo basi, tunazingatia mabadiliko yetu ya kihistoria na kuendana na mabadiliko, uaminifu kwa umma, kufikia eneo kubwa kijiografia, muunganisho wa kimataifa na uwezo wa kuhusisha kukutana ana kwa ana na kwa njia ya mtandao. Lengo letu kuu ni kudumisha jukumu la kihistoria la posta kama mhusika mkuu kwenye soko katika kutoa bidhaa na huduma zinazohitajika na watu binafsi, viwanda, biashara, mashirika ya maendeleo, Serikali na taasisi za ndani na kimataifa na hivyo kuchangia kwa njia mbalimbali maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika nchi yetu.

Kwa sasa tuko katika hatua ya juu katika kufanya mabadiliko kwenye shirika letu, vituo vyetu vingi vilivyowekwa kimkakati vimekarabatiwa na kuunganishwa na Mkongo wa Taifa wa uhakika wa Mawasiliano kwa ajili ya mtandao salama na imara ili kusaidia mifumo na maunzilaini zetu zilizotengenezwa kiasi kwamba mtandao mzima wa posta nchini unafanya kazi.

Sambamba na hili, tumezindua majukwaa yetu mawili ambayo yanawarahisishia wanajamii ndani na nje ya Tanzania kufanya miamala ya kielektroniki, wateja wanaweza kutoa oda za bidhaa wanazotaka, kulipia mtandaoni na posta inafikisha vitu hivyo kupitia miundombinu ya serikali, Mfumo wa Kitaifa wa Anwani za Makazi na Msimbo wa Posta uliopo kote ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa sasa, Shirika la Posta Tanzania limeanzisha "Duka la mtandaoni la Stempu za kumbukumbu" kwa ajili ya biashara ya stempu kwa lengo la kumbukumbu au kama vivutio ambapo wanaovutiwa na stempu hizi wanaweza kutolea oda pia kupitia duka hili, kulipia mtandaoni na posta inawatumia ipasavyo stempu zilizotolewa oda.

Hata hivyo, shirika letu, Shirika la Posta Tanzania limeweza kupata mapato, ambayo ni matokeo ya upanuzi unaoonekana wa sasa wa biashara za mtandaoni, ukuaji wa mapato na kuongezeka kwa wateja wengi kuridhika na huduma.

Kwa mantiki hii, tunapoadhimisha Siku ya Posta Duniani leo, tunapenda kuwashukuru kwa dhati wateja wetu, wadau na umma kwa msaada mkubwa waliotupa na hivyo tumeendelea kuwa wa muhimu na kinara kwenye soko katika biashara za posta nchini.

Tumedhamiria kumtumikia kila mtu katika jamii na kwa kupitia huduma zetu za kidijitali; tunaweza kufanya, sio tu kufanya, lakini pia kufanya kwa ubora zaidi na kwa gharama nafuu ambazo kila mtu anaweza kuzimudu iwe vijijini au mijini. Inawezekana kabisa; mtandao wetu mpana ni nguzo na upo kwa maendeleo ya taifa.

**Asanteni nyote.**

**Macrice Daniel Mbodo**
**POSTAMASTA MKUU**

UREMBO

# Manukato na urembo



MAFUTA yanayotoa harufu nzuri yanayopulizwa kwenye ngozi au katika nguo, maarufu kama manukato moja ya kipodozi kinachoongeza thamani ya urembo wa mtu.

Ukitaka kuwa mrembo ni wazi unatakiwa kuuweka mwili katika hali nzuri na ya kupendeza kuanzia mwili, mavazi, mitindo ya nywele na uso.

Kuna mambo mengi ya kukufanya uendelee kuonekana mrembo, lakini mafuta ya manukato yananogesha na kuhamasisha urembo kwa watu wengine.

Wakati wa kuchagua aina ya manukato ni vyema ukatumia njia ya asili kujua ukali wa harufu na ubora wa mafuta yake.

Unatakiwa kupulizia kidogo kwenye kiganja cha mkono na kisha kunusa ili uweze kujua harufu yake kama umependezwa nayo.

Usitumie manukato ya aina fulani kwa sababu ya shinikizo la marafiki au ndugu.

Jaribu kutafuta aina ya manukato uliyoyachagua kwa sababu kuna manukato yana harufu kali ambayo huleta tabu kidogo kwa baadhi ya watu unaokuwa nao karibu.

Chagua manukato ambayo yana harufu iliyotulia na pia ukali wa manukato wakati mwingine husababisha kujipulizia kiasi kikubwa cha manukato hali ambayo huwa kero kwa wengine.

Jaribu kutumia manukato kiasi kwa sababu aina nyingine hudumu muda mrefu na unapojipulizia kwa wingi unasababisha usumbufu kwako na watu wengine.

Inashauriwa kutumia manukato ili kuondoa harufu ya mwili kutokana na kutooga au sababu nyingine hapo maana ya manukato hupotea.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Chapati za mtindi





CHAPATI za mtindi ni laini zenye protini nyingi ambazo zinafaa kuliwa siyo tu kama kifungua kinywa wakati wa asubuhi, bali pia zinafaa kuliwa hata wakati wa jioni kama chakula cha jioni.

**MAHITAJI**

Kikombe kimoja na nusu cha chai cha unga wa ngano, sukari vijiko vitatu, kijiko kimoja cha chai, kijiko kimoja cha baking soda.

Mahitaji mengine ni robo kikombe ya chumvi, maziwa mtindi kikombe kimoja na robo tatu, yai moja, vijiko viwili vya siagi, vijiko viwili vya Vanila na mafuta ya kupikia kadiri ya mahitaji yako.




**NAMNA YA KUPIKA**

Chukua bakuli kubwa, weka unga wa ngano, sukari, baking powder, baking soda na chumvi, kisha changanya vizuri.

Chukua bakuli nyingine ndogo, weka maziwa ya mgando, yai, siagi na vanila, kisha changanya kwa kupiga piga, hadi uone mchanganyiko huo umechanganyika vizuri.

Mimina mchanganyiko huo wa maziwa ya mgando, yai, siagi na vanila kwenye bakuli kubwa lenye mchanganyiko wa unga wa ngano, sukari, baking powder, baking soda na chumvi, kisha changanya kwa kupiga piga na hadi uone mchanganyiko huo umechanganyika vizuri.

Weka kikaango kwenye jiko lenye moto wa wastani. Weka kijiko kimoja cha chai cha mafuta ya kupikia kwenye kikaango, kisha yasambaze vizuri.

Mimina robo kikombe cha uji wa chapati kwenye kikaango na usambaze vizuri uji huo kwa kutumia kijiko.

Kaanga upande huo wa kwanza wa chapati kwa muda wa dakika tatu, au hadi utakapoona umeiva na kuwa na rangi ya kahawia, kisha geuza na ukaange upande wa pili kwa muda wa dakika moja au tano hadi kuwa na rangi ya kahawia.

Epua chapati na uiweke kwenye sahani tayari kwa kula na unaweza kula kwa chai, juisi, soda au kimiminika kingine.

## MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya

### Jinsi ya kusafisha sofa ya kitambaa



KUSAFISHA sofa ni jambo la muhimu si kwa ajili ya kuondoa uchafu ulioganda kwenye kitambaa, bali ni kuweka mwonekano safi na maridadi.

Kuna njia mbalimbali za kusafisha sofa ya kitambaa lakini zipo chache muhimu na zinapendekezwa kuzifuata pale unapotaka kusafisha ukiwa nyumbani.

**1:** Tumia mashine ya kuoshea sofa, anza kwenye mito na kisha safisha sofa lote.

**2:** Unaweza kutumia sabuni lakini inahitaji umakini katika kufuta, muhimu tumia kitambaa chenye povu la sabuni kwa ajili ya kufutia uchafu ulioganda.

**3:** Tumia brashi kusugulia uchafu na kisha kwa muda wa dakika 30 na kisha tumia kitambaa kufuta uchafu.









# Mambo ya kuzingatia unapotafuta eneo la kujenga nyumba

KUTAFUTA ardhi ni hatua ya awali ambayo mtu hufanya katika kuelekea kujenga nyumba ya ndoto yake bila kujali mahali alipoipata ardhi hiyo.

Pamoja na kuwa eneo la ujenzi wa nyumba linaweza kuwa mahali popote, kuna mambo ya kuzingatia. Mtaalamu wa ujenzi, Tamiko Hatula, anasema kuna mambo ya msingi unapochagua eneo la kujenga, ambayo mtu anapaswa kuyazingatia.

Miongoni mwa mambo hayo ni pamoja na kufanya uchunguzi wa historia ya eneo husika unalotaka kununua na kuangalia ufikikaji wake.

"Kiwanja chenye barabara pande zote huhusiana na furaha, afya njema na mafanikio. Pia huwa na hewa, mwanga na nafasi ya kutosha. Kwa kiwanja kisichokuwa na barabara pande zote, ni muhimu kuwe na barabara upande wa Kaskazini au Mashariki. Sababu ya msingi ni kwamba nyumba itakayojengwa itakuwa na mwanga na hewa ya kutosha kuanzia asubuhi," anabainisha.

Jambo lingine ambalo anashauri kuzingatia wakati wa kutafuta kiwanja kwa ajili ya ujenzi ni pamoja na kuhakikisha eneo unalonunua ni kwa ajili ya makazi au biashara na makazi.

"Hii itakusaidia uepukane na usumbufu wa kubomolewa au kuwa na hofu ya kuhamishwa. Hakikisha unafuata taratibu zote za umiliki wa ardhi zilizowekwa," anasisitiza.

Hatula anashauri pia kuepuka kununua kiwanja kinachouzwa na mtu aliyepatwa na dhiki au kufilisika kwa kuwa baadaye kinachangia kukukosesha furaha na amani. Kwa maneno mengine, kiwanja hicho kinaweza kuwa na migogoro siku za baadaye.

"Kiwanja cha namna hii ni muhimu kinunuliwe kwa uangalifu mkubwa kwa sababu endapo utanunua kwa lengo la kujinufaisha mwenyewe zaidi. Kitakufanya baadaye ukose furaha na amani na labda manung`uniko yatokanayo na muuzaji au jamii inayozunguka yatachangia kukuondolea heshima na utu," anatanabahisha.

Anashauri kuepuka kiwanja kilicho jirani au kinachopakana na maeneo ya mikusanyiko mikubwa ya kijamii zikiwamo kumbi za starehe, kanisa, msikiti, kiwanda, chuo, jeshi, shule, soko, sehemu ya stendi za magari.


Anasema maeneo haya huwa na kelele nyingi na mara nyingi matumizi yake huathiri maeneo yaliyo jirani, ikiwamo kubadilishwa kwa matumizi wakati wowote na pia ni vigumu kulea watoto na kuwakuza kimaadili katika maeneo hayo.

Mengine anayoshauri kuzingatia ni kuepuka kununua eneo linalomilikiwa au lililomilikiwa na taasisi za kiimani, kuepuka eneo lililo jirani na sehemu ya taka, lenye magofu mengi, mapingamizi, chenye nyufa na mipasuko pamoja na chenye udongo wa mfinyanzi.





# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2022
SMS - 0713 447766
PANYA!?
ATOKE WAPI!?
JUKWAANI
WAMIGEUDHWA THAMAKI NCHANGA, HAINA MBAMBAMBA! IMIISHA HIYO
MUME WANGU PUNGUZA HASIRA USIENDE HUKO SIRUDII TENA!
NI HERI NIKADANGIWE KULIKO NDANI YA NDOA NAKO NAULIZWA NNA SHING'NGAPI?
HE!
R.I.P
DORA
POLISI VIDUME BWANA! MJINI KIMYAAAA HAKUNA CHA PANYARODI WALA PANYABUKU!
ENDELEA KUWASHUKURU HIVYO HIVYO! DUME ZIMA NYUMBA INA MAGETI KILA MAHALI, LAKINI BADO ULIKUWA UNALALA 'UVUNGUNI' KULARIBA!
NILIKUWA NALAZA GARI KABLA GIZA HALIJAINGIA NSHATINGA HOMU!
HUYU MAMA MIZIMU YAKE IMEGUNDUA KAMA 'NANJUNGANJUNGA' SINA UGANGA NAUNGAUNGA
TUMEKUELEWA TUNAJADILIANA TUTARUDI
ANATAJA MILIONI ILI AKUMALIZIE SHIDA ZAKO, ANGEKUWA HANA SHIDA MBONA KAVAA 'PUPI?' HAJAVAA SUTI!
KWANI AFANDE KUMDUNDA MKE WANGU NDIO IWE NONGWA KAMA UMENISAIDIA KULIPA MAHALI?
MIMI MWENYEWE UNAVYONIONA SIJAWAHI HATA KUMSONYA! WEWE UNAMDUNDA KAMA NANI? UKIRUDIA NAKUJA KUKUCHAMBA UCHAMBIKE...
NO NO NO!!! SITAKI KUKUSIKILIZA NAJUA UMENILETEA UMBEA!
JIFUNZE KUMUHESHIMU ANAYEKULETEA UMBEA, TUNANUSURIKA VIFO KWA AJILI YA KUYAPATA MSIYOYAJUA... 'MUDY SMATI MUUZA VIJORA UNAMJUA VIZURI? NIULIZE KAFANYAJE...
...KINYUNYIZO CHA LEO...
KONA YA BARABARA HAINA GOLI WALA REFA

# Daraja lalipuliwa Crimea, Russia yaapa kulipa kisasi

**MOSCOW,** Russia

RUSSIA imetangaza kuwa daraja linaloiunganisha na rasi iliyoichukua ya Crimea limeharibiwa kufuatia mlipuko wa lori uliosababisha moto mkubwa.

Hata hivyo, imeapa kuwakamata washukiwa, lakini ilijizuia kuitaja Ukraine

Katika taarifa yake, Russia ilisema mlipuko huo wa bomu kwenye lori ulisababisha moto uliochoma mabehewa saba ya mafuta yaliyokuwa yakisafirishwa kwa treni na pia kusababisha sehemu za miundombinu hiyo inayojumuisha barabara na reli kuharibika.

Daraja hilo lenye urefu wa kilomita 19 inayounganisha bahari Nyeusi na bahari ya Azov lina vituo vya treni na vya magari.

Picha na video zilizosambaa kwenye mitandao ya kijamii zilionesha moto mkubwa kwenye daraja hilo na kusababisha sehemu kuporomoka hadi baharini.

Mashirika ya habari ya Russia yameinukuu kamati ya kitaifa ya kupambana na ugaidi ikithibitisha kisa hicho na kuongeza kuwa bomu lililokuwa kwenye gari lililipuka kwenye daraja hilo la Crimea jana asubuhi na kusababisha moto ulioteketeza mabahewa saba ya mafuta.

Daraja hilo lililozinduliwa rasmi na Rais Vladimir Putin mwaka 2018, ni kiungo muhimu cha kupitisha zana za kivita, zinazopelekewa kwa wanajeshi wa Russia wanaopambana nchini Ukraine.

Awali, Russia ilishikilia kuwa daraja hilo ni salama licha ya vita vya Ukraine.

Spika wa jimbo la Crimea aliituhumu Ukraine kuhusika na mlipuko huo

Spika wa bunge linaloungwa mkono na Russia katika jimbo hilo la Crimea aliituhumu Ukraine moja kwa moja kuhusika na mlipuko huo, lakini Russia haikutoa tuhuma.

Mara kwa mara maofisa wa Ukraine wamekuwa wakitishia kushambulia daraja hilo. Punde tu baada ya mkasa ulioharibu daraja hilo, baadhi ya maofisa wa Ukraine walipongeza.

Ofisa mkuu katika Ikulu ya Ukraine Andrii Podolyak alichapisha kwenye ukurasa wake wa Twitter, picha iliyoonesha sehemu kubwa iliyoporomoka ya daraja hilo, kisha akaandika, "daraja la Crimea, huu ni mwanzo. Kila kitu ambacho ni kinyume cha sheria sharti kiharibiwe. Kila kitu kilichoibiwa sharti kirudishiwe Ukraine na kila kitu kinachokaliwa na Russia kiondolewe".

Kumekuwa na milipuko kadhaa katika vituo vya kijeshi vya Russia katika rasi ya Crimea.

Ikiwa itathibitishwa kuwa Ukraine imehusika katika mlipuko wa hivi karibuni, basi itaashiria hali tofauti ikizingatiwa daraja hilo liko mbali na uwanja wa mapambano.

Japo Russia ilikamata baadhi ya maeneo ya kaskazini mwa rasi ya Crimea mwanzoni mwa uvamizi wake nchini Ukraine na kujenga njia kufikia Bahari ya Azov, Ukraine inaendeleza mashambulizi yanayolenga kuyakomboa maeneo hayo.

watu 14 wafariki Ukraine

Wakati huo huo, idadi ya watu waliouawa kufuatia shambulizi la makombora ya Russia katika mji wa Zaporizhzhia kusini mwa Ukraine, imeongezeka na kufikia 14.

Mamalaka katika mji huo ilisema makombora hayo yalipigwa kabla ya mapambazuko siku ya Alhamisi huku matatu kati ya hayo yakitua katikati mwa mji huo wa kimkakati. Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky, katika mtandao wake wa telegram aliandika Zaporizhzhia inakabiliwa na mashambulizi makubwa ya roketi kila siku na kuongeza kuwa huo ni uharibifu wa makusudi.

Mji huo ambao bado upo chini ya udhibiti wa Ukraine ni eneo ambalo kinu kikubwa cha nyuklia barani Ulaya kinapatikana huku eneo hilo likikabiliwa na mapambano na kurushwa kwa makombora karibu na eneo hilo.

Hata hivyo mamlaka ya Russia inadai kuwa tayari imetwaa eneo hilo ingawaje vikosi vyake havidhibiti eneo lote **DW**



Moto ulioambatana na moshi mzito ukionekana kwenye daraja lenye urefu wa kilomita 19 linalounganisha Crimea na Russia baada ya lori lilobeba bomu kulipuka. PICHA: REUTERS

## Lithuania yadai Belarus inawasaidia wahamiaji

**VILNIUS,** Lithuania

WALINZI wa mpakani katika eneo la Baltic wamesema vikosi vya ulinzi vya Belarus vimewasaida wahamiaji kuvuka kinyume cha sheria kuingia katika taifa jirani la Lithuania.

Kulingana na walinzi hao, maofisa wa Belarus walikata uzio wa waya wa mpaka na kuwaruhusu wahamiaji kuvuka mpaka kwa ajili ya kuelekea nchi za Ulaya.

Hata hivyo muda mfupi baadae kundi la wahamiaji hao lilidhibitiwa baada ya kuingia upande wa pili wa nchi, wakati walinzi wa Belarus walijificha vichakani.

Lithuania ina mpaka wa karibu kilomita 680 na Belarus, ambao ni sehemu ya mpaka wa nje wa Umoja wa Ulaya.

**DW**

## Mbunge asimamishwa kutaja kunyoa nywele za siri

**LUSAKA,** Zambia

MBUNGE mmoja nchini Zambia amepewa adhabu ya kusimamishwa kazi kwa muda wa mwezi mmoja baada ya kutaja nywele za sehemu za siri.

Kukata nywele za sehemu za siri kwa watu wazima ni desturi nchini Zambia, kwani watu wenye nywele ambazo hazijakatwa huchukuliwa kuwa wachafu.

Hata hivyo, kuzungumzia nywele hizo katika maeneo ya umma ni kinyume na mila za waafrika.

Munir Zulu Jumatano alikasirishwa baada ya Jamba Machila, kutoka chama tawala cha United Party for National Development kumtaja kama kijana wakati wa mjadala wa wabunge kuhusu kufutwa kazi kwa wakuu wa wilaya.

"Kila mmoja wetu hapa ananyoa nywele za sehemu za siri, sisi ni wazee."

Matamshi hayo yaliibua hisia kali kutoka kwa wabunge wengine waliompigia simu Spika Nellie Mutti, kumshinikiza Zulu kuondoa taarifa hiyo.

Wabunge hao walisema walihisi wametukanwa.

Katika hekaheka iliyofuatia, mbunge mmoja alisikika akimtaja Zulu kama panya.

Zulu baadaye aliambia BBC kwamba haoni kosa kutumia neno nywele za sehemu za siri kwa sababu lilitumiwa kwa njia ya staha kuwaelezea watu wazima.

Alisema amepewa nafasi ya kuthibitisha kwamba hakufanya kosa lakini kabla ya suala hili kwenda kwenye kamati ya marupurupu kama utaratibu, alisimamishwa kazi kwa muda wa mwezi mmoja.

"Kusimamishwa huku ni kidogo, kulipiza kisasi na hakuna mfano," alisema

Aliongeza "Tuna bunge la aina gani ambako naweza kujulikana kama panya na hakuna kinachofanyika badala yake naulizwa kuhusu matamshi yangu?"

Zulu, sio mgeni katika mabishano. Hapo awali amepigwa marufuku kutoka bungeni kwa kuvaa vazi la thobe ambalo lina kifundo cha mguu mara nyingi huvaliwa na watu wa Mashariki ya Kati na Afrika Kaskazini.

**BBC**

MAKALA

# WALIMU MAENEO YA PEMBEZONI WATAZAMWE KWA NAMNA YA PEKEE



Na Magabilo Masambu

NI ukweli kwamba nchi yetu ni kubwa na pengine inaweza kuonekana kwamba rasilimali tulizo nazo hazitoshelezi kuboresha maisha ya watu kwa kiwango ambacho kila mtu atаridhika. Lakini waswahili wanasema kupanga ni kuchagua, hivyo kama nchi lazima tuwe na vipaumbele. Inawezekana mambo yote yakawa muhimu lakini kuna ya muhimu zaidi.

Elimu katika taifa lolote lazima kiwe kipaumbele cha kwanza kabisa, kwa sababu mambo mengine yote hutokana na elimu. Hatuwezi kuwa na taifa imara kama mfumo wa elimu si imara. Mfumo wa elimu pekee hautoshi, hivyo lazima tuwe na watu walio tayari kuutekeleza na katika kuutekeleza, lazima kuwe na mazingira mazuri ya utekelezaji.

Mtekelezaji wa kwanza wa mfumo wa elimu ni mwalimu ambaye amepewa mamlaka ya kisheria katika utekelezaji wa mtaala wa elimu. Serikali inasimamia utekelezaji huo na wanafumzi ni wapokeaji wa maarifa yaliyomo katika mtaala huo.

Kwa hiyo, serikali pamoja na kwamba inayo mamlaka ya kuhakikisha mtaala unatekelezwa, pia inao wajibu wa kuhakikisha mazingira ya ufanyaji kazi wa watumishi katika sekta nzima ya elimu yanaboreshwa na kuwa rafiki kwa watekelezaji.

Ni kweli kwamba juhudi mbalimbali zimefanyika, lakini nadhani bado yanahitajika mapinduzi makubwa katika kuhakikisha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji yanakuwa mazuri zaidi kwa walimu na wanafunzi, ili elimu itokanayo na utekelezaji huo, iwe na tija kwa wahitimu na kwa taifa vilevile.

Hivi karibuni, vijana wetu wamehitimu elimu ya msingi ambayo kimsingi ndiyo ufunguo wa elimu kwa kila mtahiniwa kwa ajili ya kusonga katika ngazi nyinginezo za elimu, lakini ukijaribu kutazama maeneo mengi hasa vijijiji, bado kuna changamoto za kimazingira za kujifunzia na kufundishia.

Walimu katika maeneo hayo ya vijijini na pembezoni mwa miji, watazamwe kwa namna ya pekee. Pengine wizara ya elimu na serikali kwa ujumla watenge fedha za kuwalipa walimu posho.

Siwezi kuziita posho za mazingira magumu lakini itoshe kusema kuwepo na fedha za ziada zaidi ya mishahara yao wanayoipata, ambayo inafanana na wale wanaoishi maeneo ya mjini.

Kuna wakati walimu hawa wanasafiri umbali mrefu kufuata huduma za kiofisi kwa kutumia gharama kubwa kama nauli, ambazo zinatoka kwenye mshahara uleule na kufanya maisha yao kuwa chini, jambo linalowafanya washindwe kupiga hatua za kimaendeleo.

Kuna uhusiano wa karibu sana kati ya utulivu wa nafsi na utendaji kazi mzuri na wenye tija. Kama walimu hao watakuwa wanawaza zaidi juu ya namna gani watajikwamua katika mazingira magumu, ina athiri pakubwa katika utendaji wao wa kazi na mwisho wa siku wanafunzi wanashindwa kupata kinachowastahili.

Ni kweli kwamba miundombinu ya kufundishia na kujifunzia ni muhimu sana ndiyo maana serikali inaweka nguvu kubwa katika kujenga madarasa ili kukabiliana na wingi wa vijana wanaoongezeka kila mwaka.

Ni muhimu sasa ujenzi huu wa madarasa uendane na ujenzi wa nyumba za walimu ili kuondoa adha ya walimu kudaiwa kodi huko mtaani. Kuna mazingira mwalimu anaweza kupangiwa kituo na hakuna hata nyumba za kupanga zaidi ya nyumba chache za wenyeji, jambo linalomlazimisha kupanga mbali na eneo lake la kazi.

Inawezekana hatupati elimu ya pamoja au watoto wetu si walimu, kwa hiyo kuziona changamoto hizi inakuwa ngumu. Pamoja na hayo yote ni muhimu kuelewa kwamba walimu wengi wanapitia changamoto nyingi hasa hawa walio pembezoni mwa miji kiasi cha kuwafanya wengine wawe na msongo wa mawazo na kutumia muda mrefu kuwaza namna gani watatoka huko.

Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) inaweza kuwa shahidi wa namna walimu wanavyopambana kutoka katika maeneo ya pembezoni kuhamia mjini. Lakini ikiwa walimu hao watapata posho ya ziada au wakajengewa nyumba, huo usumbufu wanaoupata TAMISEMI wa kujibu barua za walimu kila siku, kwa kiasi kikubwa utafutika na walimu watatumikia kwa moyo wa dhati kabisa.

Huko pembezoni pia kuna Watanzania wanaohitaji huduma za elimu na hivyo tusingependa kuona walimu wanahama na kuwakimbia watanzania wenzao, jambo la muhimu ni serikali kuboresha mazingira na masilahi ya walimu hao, ili watanzania hao waendelee kuelimika.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Kisa cha mwanamuziki aliyeuawa kwa mapanga sababu ya nyumba ndogo - 2*



Na Adam Fungamwango

WIKI iliyopita tulimzungumzia mwanamuziki maarufu wa zamani wa Kenya, George Mukabi, aliyezaliwa 1930 nchini humo na kufariki dunia kwa kuuawa kinyama mwaka 1963 akiwa na umri mdogo tu wa miaka 33.

Hadi anafariki dunia, alikuwa ametunga na kuimba nyimbo nyingi, lakini hapa Tanzania kuna nyimbo zake zilizopendwa sana na kupigwa kwenye redio, santuri na kwenye sherehe mbalimbali za kijamii kiasi cha kumpatia sifa kubwa. Miongoni mwa nyimbo hizo ni 'Sengula Nakupenda', 'Kweli Ndugu' na 'Mtoto si Nguo'.

Mashairi ya nyimbo hizo tuliyaweka wiki iliyopita. Kwa kifupi tu kabla hatujamalizia kwenye kisa cha kuuawa kwake ni kwamba Mukabi alikuwa ni wale wanamuziki wa mwanzo miaka ya 50 hadi 60 waliokuwa wakipiga magitaa baridi maarufu kama magalatoni, na yalikuwa yakihanikizwa na mipigo ya chupa, manyanga, mbao, bati bao au kitu chochote kile kitakachokuwa kikisindikiza gitaa, kimuziki inafahamika kama 'timing'.

Nyimbo nyingi za aina hiyo zilivuma sana wakati ule kabla na baada ya uhuru na studio za kurekodia nyimbo hizo ambazo zilikuwa nchini Kenya. Ukanda wote wa Afrika Mashariki na Kati, Kenya ndiyo ilikuwa kama kituo kikuu cha wanamuziki wengi kutoka Tanzania, Zaire (sasa Congo DR), Zambia, Zimbabwe na hata Afrika Kusini, walikuwa wanarekodia nyimbo zao nchini humo na kutengenezwa santuri ambazo wakati huo zilikuwa zinaitwa GV.

Tuje kwenye kifo chake ambacho kilileta huzuni, simanzi, taharuki na wasiwasi mkubwa kwa mashabiki wake na wa muziki Afrika Mashariki na Kati kwa ujumla. Kulikuwa na uvumi mwingi, ikiwemo kuwa alioa mke, baada ya siku chache mke akamkimbia akarudi kwao, akaamua kumfuata na huko akauawa na mahawara wa mkewe.

Nadhani hicho ndiyo kisa hata utunzi wa wimbo wa John Mwale ambao tulianza nao wiki iliyopita.

"Kuoa tunaoa lakini tukumbuke yaliyotendeka kwa George Mukabi, George alipoona bibi akakimbia, kwa kumfuata akauawa bure. Wazazi wa Mukabi walipata hasara, kupoteza mali na mtoto wao, wale ambao hatujaoa kweli ndugu zangu, tukifikiri hilo hatutooa tena."

Hata hivyo, Jeshi la Polisi nchini Kenya baada ya kufanya uchunguzi wake liligundua kisa cha kifo chake hiki.

Baada ya kupiga muziki wake kwenye jiji la Nairobi, alirejea kwao Kakamega na kufikia nyumbani kwa mke mdogo. Akaweka gita lake na kumwambia anakwenda kulala kwa mke mkubwa. Mke mdogo wivu ukamshika. Kitendo cha kufikia kwake kuweka gitaa, halafu aende kulala kwa mke mkubwa hakikumuingia akilini, pamoja na wivu, akadhani pia pesa zote alizopata kwenye muziki huko mjini anakwenda kupewa mke mkubwa.

Wakati Mukabi anaondoka, mke mdogo akaamua kuchukua gitaa la mumewe na kulivunja. Ikumbukwe lilikuwa ni gitaa jipya kabisa la kisasa wakati huo ambalo alipewa na rafiki yake raia wa Uingereza.

Aliposikia kama kuna sauti za kuvunja kitu, akarejea na kukuta gita lake limevunjwa. Mke akaamua kukimbilia kwao. Mukabi kwa hasira na yeye akamfuata. Mke alipofika kwao akakimbilia moja kwa moja chumbani kwa baba yake. Mukabi akaingia humo humo. Baba mkwe alikuwa nje na aliona timbwili lile. Bila kufikiria akaanza kupiga yowe kuita majirani wamsaidie.

Wanakijiji walipofika hawakuuliza, wakaanza kumpiga Mukabi kwa mapanga, mawe, rungu shoka na kila aina ya silaha za jadi. Binafsi nina wasiwasi labda aliita kelele za mwizi, na wao walipofika hawakuuliza kwa sababu ilikuwa usiku.

Kwa kujaribu kujiokoa alikimbia na kuvuka Mto Yala, lakini hakufika mbali. Aliishiwa nguvu akaanguka na kuzimia.

Bado wanakijiji wale wa Busoso waliendelea kumsaka na walipomkuta akiwa ameanguka na amezimia, wakammalizia kwa mawe kwa mara nyingine tena, mapanga, majembe na marungu, kabla kumkatakata vipande kama nyama. Sehemu ya mwili wake wakaipakia kwenye mkokoteni na kuipeleka kwenye hospitali ya Kakamega.

Lilikuwa tukio la kusikitisha sana. Lakini pia mpaka hapa kuna maswali ya kujiuliza. Je baba mkwe alipiga kelele za mwizi ndiyo maana wanakijiji walifika na kumpiga kwa hasira? Kwa nini baadaye hakuwaambia kuwa ni mkwe wangu? Kwa nini pia mke mdogo hakumtetea mumewe kwa kuwaambia si mtu mbaya au mwizi baada ya kuona anashambuliwa kwa silaha za jadi?

Kwa nini wanakijiji wa Busoso bado walizidi kumsaka, hata baada ya kukimbia ukweni hapo kuokoa maisha yake alipoona hakuna msaada wala mtu wa kumtetea na walipomkuta amezimia wakamkazia kwa kumuua tena kwa hasira? Kwa nini wanakijiji hao walikuwa na hasira zilizopitiliza hadi kumkatakata kama nyama?

Kifo hiki hakikuumiza mashabiki tu wa muziki bali hata wanamuziki wenzake ndiyo maana nyimbo nyingi zilitungwa kutokana na tukio hilo.

Mwanamuziki mmoja wa Kenya naye alitunga wimbo wa kuwashutumu wanakijiji hao akaimba. "Watu wa Busoso walikata George kama mti."

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

PRINCE Petit ni kijana aliyelelewa kwenye mazingira ya ajabu. Amelelewa na baba yake mzazi tu bila mama. Madada wa kazi waliopewa kazi ya kumlea walipewa mkataba wa mwaka mmoja tu na walipomaliza hawakuongezwa. Hakupelekwa shule yoyote ile badala yake walimu walilipwa pesa kwa ajili ya kumfundisha nyumbani tu. Hata alipokuwa akipata nafasi ya kwenda kufurahia maisha na kuitazama dunia nje ya nyumba yao, alipewa angalizo la kutozoeana na mtu yeyote yule. Aliingiziwa falsafa na vitu vingine kichwani mwake mpaka akawa na tabia ambazo ni tofauti na umri wake. Akiwa na miaka mitano tu, alianza kufundishwa kulenga shabaha na alipofikia miaka minane alikuwa na uwezo wa kutumia bastola ya aina yoyote ile na angeweza kuajiriwa kwenye shirika lolote la kijasusi duniani. Anapofika umri wa miaka 25, baba yake, Mzee Pokwa anamtuma kazi. Kazi ya kuua na kulipiza kisasi. Ni kwa nini? Anakwenda kumuua nani? Kwa nini baba anayejua mkasa mzima asiende mwenyewe? Kitu gani kilichotokea huko nyuma? Nakala yako ya Nipashe itakufanya kujua kilichopo nyuma ya pazia.

# Mwisho wa Mauaji-22

"Sasa ndugu yangu, unatuita, halafu na wewe unaua?"

"Nisingeua, ningeuawa."Akajibu.

Kitu ambacho Polisi walichogundua kuwa watu wale ndiyo wanahusiana na kesi za kuuawa kwa Sabri, Nassor Hassan na Hussein.

******************************

Mahakama Kuu kanda ilikuwa imejaa watu wengi kufuatilia kesi iliyovuta watu wengi kwenye magazeti televisheni na mitandao ya kijamii.

Ni ya Prince Petit, kijana aliyeshtakiwa kwa kuuwa watu watano ambao ni Sabri, Nassor Hassan na Hussein na Pokwa.

Sababu za kuua zimeelezwa kwa kirefu kwenye magazeti, na wengi waliosoma walionekana kumuonea huruma kwani alionekana hajui alitendalo.

Alikuwa anaua watu ambao wangemsaidia. Ambao walimsubiri akue, ajitokeze wamwambie kila kitu. Akidanganywa na mtu aliyejifanya baba yake mzazi alitekeleza mauaji hayo bila kujua. Hilo ndilo lililoifanya kesi hiyo kuwa si kubwa tu, lakini kuvuta hisia za watu wengi na kusababisha mahakama kufurika watu.

Kabla haijaanza, Prince alikuwa amekaa akizungukwa na maaskari. Macho yake yalishtuka alipoona sura ya mama yake mdogo Hidaya.

"Mamaa" Akaita, na moja kwa moja Hidaya akafika alipo na kumkumbatia. "Mwanangu nimelia sana kuhusu kukamatwa kwako. Siyo kosa lako, bali lile shetani mzee Pokwa. Niko tayari kwa ushahidi."

Wakati huo huo, Hasnat naye akasogea na kumkumbatia. "Mpenzi, samahani sana, niko matatani, najua itakuwa imekukwaza sana." Prince akamwambia Hasnat.

"Hapana Prince, tatizo lako ni langu, mimi niko na wewe hadi mwisho wa hili, kwa yote yaliyotokea mwanzo tangu siku ile ulipokuja nyumbani kwa mara ya kwanza na haya yaliyoendelea, ni kwamba umepata madhila makubwa sana na nimejikuta nimetokea kukupenda." Akasema huku akitokwa na machozi. Prince akamfuta kwa mikono akamwambia

"Usilie, unaona watu wanatuangalia sana, yataisha haya."

"Mhh mwenzangu sijui kama yataisha, mimi nilitaka yaishe ili unioe." Sentesi hii ilimfanya Prince atulie kidogo. Hakuwahi kuambiwa maneno ya kuoana na Hasnat, msichana aliyetokea kumpenda. Akahisi furaha ya ajabu ghafla ambayo ilimfanya asijue hata la kufanya, kama ni kupiga kelele, kulia au kucheka.




**"Pole mwanangu, Mungu akupe tu afya, miaka miwili si mingi utatoka." Hidaya alimfariji Prince.**

"Nikifungwa?" Swali lilimtoka ghafla.

"Labda uhukumiwe kunyongwa, lakini kama ni miaka tu, nitakusubiri mpenzi wangu." Akajibu na kumfariji.

"Ngoja tuone kwanza kwenye hii kesi, lakini mdomo wako uwe wa heri, mimi pia nimejiandaa kukuoa" Akajibu na kumfanya Hasnat atabasamu, na kucheka kicheko laini, kilichochanganyikana na aibu. Prince akamgeukia mama mkwe wake mtarajiwa.

"Mama nashukuru sana kwa kuja hapa. Mimi sina ndugu yoyote hapa zaidi yenu. Nimefarijika sana japo nina kesi. Nimejawa na furaha baada ya kusikia umati wote huu, wengi wao wananipa sapoti kwa yaliyonikuta. Ila afande huyo hapo nyuma atakupa ufunguo na maelekezo yote. Ile nyumba ya Kinondoni niliyokuwa naishi kumbe ilikuwa ya baba yangu mzazi mzee Martin, nimegundua hati zake halisi ambapo alikuwa amezificha. Mtakwenda kukaa huko mkitoka hapa kama sitoachiwa. Mtakwenda kukaa humo kwa sababu ni nyumba yangu. Kumbe mzee Pokwa alikuwa na familia ya mke na watoto. Kumbe alikuwa akitoka pale kwangu anakwenda kwenye familia yake, mimi ananidanganya kuwa ni mtoto wake wa pekee. Mle ndani kuna kila kitu ambacho mtahitaji. Kama nitachukua muda mrefu sana rumande au jela iwapo nikifungwa, basi mama utaendelea tu na biashara yako, umtunze Hasnat hadi nitakaporejea." Akasema Prince akionekana ana uchungu moyoni.

Ni habari iliyomshtua Hidaya na binti yake na kuwafurahisha pia. Hawakutarajia kama watakutana na kitu kama hicho. Kwenda kuishi kwenye nyumba kubwa ya kisasa ilikuwa ni ndoto kwao.

"Ahsante mwanangu, Mungu akupe subira, yataisha haya, unaungana tena na familia yako, ambao ni sisi." Hidaya akamfariji.

"Nashukuru Mama kwa hiyo mkitoka hapa rudini Mwananyamala kuchukua vitu tu ambavyo mnaona ni vya muhimu, vile ambavyo si muhimu viacheni mhamie Kinondoni." Akasema na hapo hapo maandalizi ya kesi yakaanza, hivyo watu wote walitakiwa kukaa sehemu zao maalum kabla Jaji hajaingia.

***************************

Hukumu iliyotoka ni kwamba pamoja na yote yaliyoelezwa, lakini ukweli ulibaki pale pale Prince aliua, hivyo mahakama haikumuacha hivi hivi, ikamfunga miaka miwili jela.

Haikuchukuliwa kirahisi kwa Prince, Hidaya na Hasnat. Wote walisikitika, lakini iliwafariji kwa sababu haikuwa miaka mingi, kifungo cha maisha au kufa kwa kunyongwa. Na hiyo ilitokana na mazingira ya kesi yenyewe jinsi ilivyo.

"Pole mwanangu, Mungu akupe tu afya, miaka miwili si mingi utatoka." Hidaya alimfariji Prince.

"Ni kweli mama nimeumia kwenda kuishi miaka miwili bila kukuona wewe na Hasnat."

"Hapana, tutakuwa tunakuja kukuona gerezani siku moja moja hadi utakapotoka." Akadakia Hasnat.

"Hasnat, ni miaka miwili naenda kifungoni, panapo majaliwa na afya, nikitoka nafunga ndoa na wewe."

"Kweli?" Akauliza Hasnat kama vile hajui. Akamkumbatia na wote wawili machozi yakawatoka.

Machozi yao, yalimfanya Hidaya naye aliyekuwa akiwaangalia naye machozi kumtoka na kilio juu.

"Nakupenda Hasnat."

"Nakupenda pia Prince, nenda utanikuta nakusubiri mpenzi wangu."

Ni muda ambao karandinga lilikuwa tayari kwa safari ya kuwapeleka wafungwa gerezani.

Prince aliongozwa na askari magereza kwenda kupanda. Alipofika mlangoni akageuza kichwa. Akamtazana Hasnat. Yeye akanyoosha mkono kumuonyesha ufunguo wa nyumba ya Kinondoni na tayari ameshapewa na askari polisi.

Prince akanyoosha mkono kukubali na kumuaga. Basi linalopeleka wafungwa liliwashwa tayari kwa safari. Prince alikuwa dirishani akizidi kumtazama Hasnat kwa majonzi. Hasnat akamuacha mama yake na kulisogelea hadi dirishani akasimama na kumtazama mpenzi wake. Machozi yakamtoka. Akaanza kumuimbia.

"Nenda salama Prince mpenzi, upate neema uendako na heri. Ukumbuke nyuma ninayo majonzi, nakusubiri tuje tuoane." Ulipenya kwenye masikio ya Prince. Akajikuta anatabasamu na kuonyesha ishara ya kumbusu. Hasnat akarudisha. Tayari dereva alishaanza kuliondoa basi eneo la mahakama.

**MWISHO**



# MWIJAKU, HARMONIZE HAWAPIKIKI TENA

MWIJAKU kila siku haishiwi na mbwembwe, safari hii amemkabili Harmonize, akisema alichomfanyia Mungu anajua kwani kuna siku moja atamshtaki kutokana na mambo anayoyafanya.

Akizungumza na Bongo5, Mwijaku amesema amemuondoa kama mfuasi wake Instagram baada ya kumshauri jambo jema ambalo akilifuata anaweza kubaki katika umaarufu wake.

"Harmonize nimemshauri vitu vya msingi lakini ameniona mimi mpumbavu, yote haya nafanya kwa sababu nampenda, sitaki apotee njia, nitahakikisha anaacha mambo yasiyofaa," amesema Mwijaku.



## Banaponga watua Dar kwa kishindo

KUNDI linalofanya vyema mkoani Kigoma, True Music Banaponga, limetamba kutikisa Dar es Salaam ikiwa ni siku chache zimepita tangu walipotua jijini humo.

Kiongozi wa kundi hilo Follow Bugatti, ameliambia Nipashe kuwa kundi hilo linaundwa na vijana wanne ambao ni Young Fisi, Daltonne Gwini na Huba chini ya Meneja Simon Denis wakidhaminiwa na Bushiri Dems anayeishi Marekani.

"Tumekuja kwa kishindo hapa Dar es Salaam kwasababu mpaka sasa hakuna kundi bora kama True Music Banaponga, tumekuja kufanya kolabo na wasanii wakubwa kama Whozu, Mabantu, Beka Flavour na wengine kibao chini ya udhamini mnono wa kampuni ya Dems International Star," amesema Follow.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### RONALDO KUBAKIA UNITED

MANCHESTER United ina imani Cristiano Ronaldo, 37, atasalia katika klabu hiyo Januari kwa sababu hakuna klabu nyingine iliyojitokeza kuvutiwa na mshambuliaji huyo wa Timu ya Taifa ya Ureno. ***(ESPN)***

### AUBAMEYANG ANUKIA PSG

PARIS St-Germain wanafikiria kumnunua mshambuliaji wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang, 33, katika msimu ujao. ***(Foot Mercato)***

### NEWCASTLE YAMTAKA SANTOS

NEWCASTLE United wamefanya mazungumzo na Vasco da Gama ya Brazil kuhusu uwezekano wa kumsajili kiungo wa kati, Andrey Santos, 18, ambaye anatarajiwa kugharimu pauni milioni 30. ***(The i)***

### MADDISON ANUKIA SOKONI

KOCHA wa Leicester City, Brendan Rodgers amesema anakubali kiwango kizuri cha kiungo wa kati wa England, James Maddison, 25, kitavutia maombi kwa mchezaji huyo ifikapo Januari. ***(Mail)***

### VIVEL ATAJWA CHELSEA

CHELSEA wanatazamia kumteua Christopher Vivell kuwa mkurugenzi wa ufundi wa klabu hiyo baada ya Mjerumani huyo kutimuliwa na RB Leipzig. ***(Telegraph)***

### LOZANO KUTUA ENGLAND

WINGA wa Napoli na Timu ya Taifa ya Mexico, Hirving Lozano, 27, anaweza kuishia Manchester United au Everton msimu ujao, wakala wake wa zamani amesema. ***(Mirror)***

### BENITEZ, ALONSO WATEMWA

RAFAEL Benitez na kocha mpya wa Bayer Leverkusen, Xabi Alonso walikuwa miongoni mwa majina yanayofikiriwa kuchukua nafasi ya Steve Cooper huko Nottingham Forest kabla ya klabu hiyo kuamua kumpa mkataba mpya. ***(Mail)***

### KULUSEVSKI KUIKAMUA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur watailipa Juventus pauni milioni 30.7 kwa ajili ya kumnunua winga wa Sweden, Dejan Kulusevski mwenye umri wa miaka 22 kwa mkataba wa kudumu. ***(Calciomercato)***

### MESSI KUREJEA BARCELONA

MAKAMU wa Rais wa Barcelona, Eduard Romeu ana imani klabu hiyo inaweza kutafuta njia ya kumrejesha mshambuliaji wa Paris St-Germain na Argentina, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 35, ikiwa wanataka. ***(90min)***

### ROMEO AJIFUA BRENTFORD

MTOTO wa David Beckham, Romeo, anafanya mazoezi katika kikosi cha pili cha Brentford baada ya kumalizika kwa msimu wa Ligi Kuu Marekani (MLS). ***(Guardian)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MBAPPE AWAFUNIKA MASTAA KWA UTAJIRI

**LONDON,** England

● ● ● Amewaondoa katika nafasi ya kwanza Messi na Ronaldo ambao walikuwa wanaishikilia...

KYLIAN Mbappe anaongoza orodha ya wanasoka wanaoingiza fedha nyingi zaidi, ikiwa ni kwa mara ya kwanza mtu mwingine isipokuwa Lionel Messi au Cristiano Ronaldo kukaa katika nafasi ya juu duniani kwa miaka tisa, kwa mujibu wa jarida la Forbes.

**Forbes wanakadiria mshambuliaji huyo wa Paris St-Germain mwenye umri wa miaka 23, atapokea kiasi cha Dola za Marekani milioni 128 kwa msimu huu.**

Mchezaji mwenzake wa PSG, Messi anashika nafasi ya pili kwa kuingiza Dola za Marekani milioni 120, huku mshambuliaji wa Manchester United, Ronaldo akiwa wa tatu kwa kuingiza Dola za Marekani milioni 100.

Mbrazil Neymar na nyota wa Timu ya Taifa ya Misri na Liverpool, Mohamed Salah wanamalizia tano bora.

Mshambuliaji wa PSG, Neymar atapokea kiasi cha Dola za Marekani milioni 87 msimu huu akiwa nafasi ya nne na Salah atapata Dola za Marekani milioni 53 akishika nafasi ya tano. Mchezaji wa mwisho kuongoza orodha hiyo isipokuwa Ronaldo au Messi alikuwa nahodha wa zamani wa England, David Beckham mwaka 2013.

Mbappe alisaini mkataba mpya wa miaka mitatu na PSG, Mei mwaka huu, ambao ulimaliza uvumi kuhusu kuhamia Real Madrid majira ya joto.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia na Ufaransa ameshinda mataji 11 katika klabu hiyo, yakiwamo mataji manne ya Ligue 1, tangu ajiunge hapo akitokea Monaco mwaka 2017.

Erling Haaland, ambaye amefunga mabao 19 katika mechi 12 akiwa na Manchester City tangu kuhama kwake kutoka Borussia Dortmund majira ya joto, anaingia kwa mara ya kwanza katika 10 bora akiwa nafasi ya sita.

Mshambulizi huyo wa Norway ni mmoja wa wachezaji wanne wa Ligi Kuu England walio katika 10 bora pamoja na Ronaldo, Salah na mchezaji mwenzake wa Manchester City, Kevin de Bruyne.

Haaland na Mbappe ndio wachezaji pekee kwenye orodha hiyo walio na umri wa chini ya miaka 30.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 367,

MECHI KALI
ARSENAL
VERSUS
LIVERPOOL
1 | 2.56
X | 3.50
2 | 2.48

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# RIBERY KUSTAAFU SOKA



**ROME,** Italia

KIUNGO wa zamani wa FC Bayern Munich na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Frank Ribery, amepanga kustaafu soka akiwa na umri wa miaka 39.


Kiungo huyo ambaye kwa sasa anaichezea Salernitana inayoshiriki Ligi Kuu Italia maarufu Serie A, amepanga kuvunja mkataba na klabu hiyo ili aweze kustaafu soka baada ya kuitumikia kwa mwaka mmoja akitokea Fiorentina.

Ribery ambaye alipata umaarufu zaidi akiwa Bayern Munich ambapo alicheza kwa mafanikio makubwa pamoja na pacha wake, Arjen Robben.

Kwa pamoja walishinda kila taji kwenye ngazi ya klabu kwa miaka 12 waliyoitumikia miamba hiyo ya soka nchini Ujerumani kabla ya kutimkia Fiorentina ya nchini Italia mwaka 2019.

Ribery atakumbukwa zaidi mwaka 2013 ambapo alikua na msimu bora zaidi na kufanikiwa kufanikiwa kuwa Mchezaji Bora wa Ulaya na kushika nafasi ya tatu kwenye tuzo za Ballon dor.

Pia alifanikiwa kuisaidia klabu yake kushinda mataji matatu ndani ya msimu mmoja wa 2012/13.



## *United yawania mabeki Inter*

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United imeripotiwa kuwania mabeki katika dirisha dogo la Januari, na wanadaiwa kutaka kuwanunua wachezaji watatu wa Inter Milan, Skriniar Milan, Alessandro Bastoni na Denzel Dumfries.

Skriniar anachukuliwa kuwa bidhaa ya moto zaidi katika nafasi ya beki wa kati na hivi karibuni alitakiwa kwa dau la Euro milioni 60 na vigogo wa Ufarasa, Paris Saint-Germain.

Inter ilikataa ombi hilo, lakini kwa kuwa mkataba wa raia huyo wa Slovakia unatarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu huu, hii itakuwa fursa yao ya mwisho kupata fedha ikiwa wanaamini Skriniar hatasaini nyongeza.

Watatu hao ndio kitovu cha mabao ya Inter msimu huu, lakini wamekaa nafasi ya tisa kwenye Serie A na kushinda mara nne na kupoteza mara nne kutoka kwa mechi nane za kwanza.

Gazzetta dello Sport inadai kuwa klabu hiyo ya Old Trafford italazimika kushindana na Tottenham Hotspur na Manchester City katika harakati zao za kumsaka Bastoni, na Calciomercato limeongeza kuwa Chelsea pia wanavutiwa na Muitaliano huyo.

## HABARI MICHEZO

,741,460

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

**BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13**

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 11/10/22 | 22:00 | Dinamo Zagreb vs RB Salzburg | 2.74 | 3.28 | 2.44 |
| 02. 11/10/22 | 22:00 | AC Milan vs Chelsea | 2.93 | 3.33 | 2.28 |
| 03. 12/10/22 | 17:15 | FC Andorra vs Burgos | 2.24 | 3.02 | 3.32 |
| 04. 12/10/22 | 22:00 | Racing Santander vs Zaragoza | 2.85 | 2.95 | 2.65 |
| 05. 13/10/22 | 03:45 | Corinthians vs Flamengo | 2.87 | 3.16 | 2.30 |
| 06. 13/10/22 | 19:45 | Betis vs Roma | 2.28 | 3.41 | 2.95 |
| 07. 13/10/22 | 19:45 | Union Saint Gilloise vs Sporting Braga | 2.34 | 3.35 | 2.90 |
| 08. 13/10/22 | 19:45 | Nantes vs SC Freiburg | 3.06 | 3.41 | 2.22 |
| 09. 13/10/22 | 19:45 | Slovan Bratislava vs FC Basel | 2.90 | 3.30 | 2.37 |
| 10. 13/10/22 | 19:45 | Djurgardens IF vs KAA Gent | 3.05 | 3.39 | 2.24 |
| 11. 13/10/22 | 22:00 | Trabzonspor vs Monaco | 3.14 | 3.39 | 2.24 |
| 12. 13/10/22 | 22:00 | Ferencvaros TC vs Red Star Belgrade | 2.23 | 3.40 | 3.05 |
| 13. 13/10/22 | 22:00 | Steaua Bucuresti vs Silkeborg | 2.70 | 3.25 | 2.55 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMAPILI - 09/10/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 3415 | Torino vs Empoli | 1.72 | 3.57 | 4.56 |
| 14:00 | 3729 | Montpellier vs Monaco | 3.53 | 3.78 | 1.90 |
| 14:30 | 2409 | Mechelen vs Anderlecht | 3.63 | 3.68 | 1.90 |
| 15:00 | 1858 | Aarhus vs Midtjylland | 2.98 | 3.32 | 2.28 |
| 15:00 | 2958 | Valladolid vs Betis | 2.80 | 3.30 | 2.44 |
| 15:30 | 1599 | Feyenoord vs Twente | 1.65 | 3.92 | 4.57 |
| 16:00 | 1027 | Udinese vs Atalanta | 2.48 | 3.28 | 2.68 |
| 16:00 | 1160 | Brest vs Lorient | 2.30 | 3.34 | 2.94 |
| 16:00 | 1186 | Salernitana vs Verona | 2.38 | 3.36 | 2.76 |
| 16:00 | 1364 | Crystal Palace vs Leeds | 2.05 | 3.46 | 3.31 |
| 16:00 | 1444 | Nice vs Troyes | 1.71 | 3.68 | 4.57 |
| 16:00 | 2374 | Malmo vs IFK Varnamo | 1.23 | 5.44 | 9.51 |
| 16:00 | 2532 | West Ham vs Fulham | 1.72 | 3.77 | 4.26 |
| 16:00 | 3225 | Angers vs Strasbourg | 2.58 | 3.33 | 2.58 |
| 16:00 | 4062 | Monza vs Spezia | 1.84 | 3.52 | 3.97 |
| 16:00 | 4830 | Clermont Foot vs AJ Auxerre | 2.06 | 3.34 | 3.44 |
| 16:30 | 2484 | Stellenbosch vs Kaizer Chiefs | 3.20 | 2.75 | 2.50 |
| 16:30 | 4876 | Monchengladbach vs FC Koln | 1.96 | 3.67 | 3.37 |
| 16:30 | 5571 | Torpedo Moscow vs Nizhny Novgorod | 2.62 | 3.16 | 2.62 |
| 17:00 | 2885 | Dynamo Kiev vs Rukh Vinnyky | 1.25 | 5.26 | 9.34 |
| 17:00 | 5884 | Kilmarnock vs Hearts | 3.23 | 3.38 | 2.13 |
| 17:15 | 4079 | Cadiz CF vs Espanyol | 2.89 | 3.04 | 2.54 |
| 17:30 | 4468 | FC Lugano vs FC Basel | 2.64 | 3.48 | 2.45 |
| 17:45 | 1100 | Heerenveen vs PSV Eindhoven | 4.95 | 4.26 | 1.55 |
| 18:00 | 3709 | Viking vs Lillestrom | 2.18 | 3.43 | 3.08 |
| 18:00 | 4254 | Rapid Vienna vs Austria Vienna | 2.03 | 3.50 | 3.11 |
| 18:05 | 4034 | Rennes vs Nantes | 1.50 | 4.29 | 5.78 |
| 18:10 | 4702 | HNK Gorica vs HNK Rijeka | 2.12 | 3.36 | 3.02 |
| 18:30 | 1101 | Djurgardens IF vs BK Hacken | 1.88 | 3.60 | 3.45 |
| 18:30 | 1629 | Hertha BSC vs SC Freiburg | 2.92 | 3.32 | 2.29 |
| 18:30 | 3243 | Arsenal vs Liverpool | 2.56 | 3.50 | 2.48 |
| 18:30 | 5453 | AIK Football vs Helsingborg | 1.44 | 4.28 | 5.83 |
| 19:00 | 1346 | AS Trencin vs Slovan Bratislava | 3.82 | 3.68 | 1.76 |
| 19:00 | 1642 | Rostov vs FC Krasnodar | 1.93 | 3.56 | 3.56 |
| 19:00 | 1857 | Cremonese vs Napoli | 6.33 | 4.55 | 1.42 |
| 19:00 | 3543 | Aris Limassol vs AEK Larnaca | 2.46 | 3.25 | 2.80 |
| 19:00 | 4613 | Shamrock Rovers vs Shelbourne | 1.39 | 4.10 | 7.22 |
| 19:00 | 4710 | Randers vs Brondby | 2.33 | 3.34 | 2.89 |
| 19:30 | 2852 | Real Sociedad vs Villarreal | 2.45 | 3.24 | 2.84 |
| 19:30 | 3761 | Charleroi vs Standard Liege | 2.13 | 3.55 | 3.10 |
| 20:00 | 5903 | Fenerbahce vs Fatih Karagumruk | 1.38 | 4.88 | 6.77 |
| 20:30 | 4449 | FK Vozdovac vs Partizan | 4.65 | 3.68 | 1.63 |
| 20:30 | 5171 | Stuttgart vs Union Berlin | 2.53 | 3.08 | 2.78 |
| 21:00 | 1953 | Everton vs Manchester Utd | 3.31 | 3.36 | 2.08 |
| 21:15 | 3803 | Aris Salonica vs AEK Athens | 2.79 | 3.03 | 2.59 |
| 21:30 | 1778 | Inter Miami CF vs Montreal Impact | 2.50 | 3.69 | 2.58 |
| 21:45 | 1121 | Roma vs Lecce | 1.34 | 4.75 | 8.31 |
| 21:45 | 1910 | Lille vs Lens | 2.36 | 3.49 | 2.74 |
| 22:00 | 2261 | Barcelona vs Celta Vigo | 1.32 | 5.11 | 8.39 |
| 22:30 | 1928 | Sporting Braga vs GD Chaves | 1.27 | 5.55 | 9.32 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# YANGA YAPANIA KUMALIZA UBABE WA SIMBA QUEENS

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga Princess, Edna Lema, amesema kikosi chake kinaendelea kufanya maandalizi bora kwa ajili ya kukiimarisha ili kuhakikisha wanafanya vizuri katika msimu mpya wa 2022/2023 wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania.

**Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam, Lema alisema kikosi chake tayari kimeshaingia kambini kuendelea na mazoezi kwa sababu anataka kuandaa timu yenye ushindani.**

Lema alisema mbali na kusajili wachezaji bora pia anahitaji kuona anakuwa na kikosi imara kitakachompa matokeo chanya katika michezo yao ya Ligi Kuu ya Wanawake watakaocheza katika msimu ujao.

"Msimu uliopita tulishindwa kutimiza malengo yetu ya kutwaa ubingwa, tumefanya usajili wa wachezaji bora watakaoleta ushindani mkubwa katika mechi zetu zote za ligi, tumeimarisha kila idara," alisema Lema.

Aliongeza anaendelea na mazoezi ya kutengeneza muunganiko wa kikosi kwa sababu amesajili wachezaji 11 wapya ambao wanatakiwa kufahamu falsafa ya timu hiyo.

"Tuna kazi kubwa ya kuandaa kikosi chetu, kitakachopambana kupata matokeo chanya pale ligi itakapoanza ," kocha huyo alisema.

Aliongeza pia watacheza mechi mbalimbali za kirafiki zitakazowajenga na hatimaye kwenda kuuzima ufalme wa Simba Queens ambao wametwaa taji la ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake kwa misimu minne mfululizo.

Yanga Princess ilipata ushindi wa bao 1-0 katika mechi ya kirafiki dhidi ya Baobab Queens iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam juzi.



Mchezaji wa Mabibo FC, Athumani Sungo (kushoto), akiwania mpira dhidi ya nyota wa Tanesco, Salum Bure, katika mechi ya bonanza la kumwenzi Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere lililoandaliwa na Taasisi ya Dira Society Group kwenye Uwanja wa Magomeni Kota, Dar es Salaam jana. **PICHA : JUMANNE JUMA**

# Yanga, Al Hilal hakuna mbabe

INATOKA UK. 24

jezi zao za rangi nyeusi, kijani na njano, walifika nusu ya uwanja.

Saa 9:12 Fei Toto ndio alikuwa mchezaji wa Yanga kuanza kukanyaga nyasi za uwanja akifuatiwa na Shaban Djuma na baada ya hapo wachezaji wengine waliendelea kuingia kwa ajili ya kufanya mazoezi mepesi ya kujiandaa na mchezo huo uliochezeshwa na waamuzi kutoka Rwanda.

Kwa upande wa Al Hilal waliongozwa na magokilipa wao kuingia kwa ajili ya kupasha huku wachezaji wa ndani wakiingia katika eneo hilo la kuchezea ili kufanya mazoezi mepesi ilipofika saa 9:17.

**IBENGE ATETEMA**

Baada ya mechi kumalizika, Kocha Mkuu wa Al Hilal, Florent Ibenge, alienda kusalimiana na Mayele na kumpongeza kwa kufanikiwa kuifungia timu yake bao.

Ibenge alionyesha ishara ya kutetema jambo ambalo lilimfanya mshambuliaji huyo Mkongomani kucheka.

# Phiri kuongoza 'mauaji' Angola

INATOKA UK. 24

Aliongeza anaamini wachezaji wake watakuwa makini na kujituma katika muda wote wa mechi ili kupata ushindi na kujiweka kwenye mazingira mazuri ya kusonga mbele.

Naye starika tegemeo kwa sasa katika kikosi hicho, Moses Phiri, alisema amezinyaka baadhi ya siri za wapinzani wao kwa kufahamu uwezo na udhaifu wao kupitia kwa marafiki zake wawili ambao ni wachezaji wa Red Arrows ambao walicheza nayo katika hatua ya awali.

**Michezo**

Jumapili Oktoba 9, 2021

Nipashe



**Mbappe awafunika utajiri mastaa**

UKURASA 21



Mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele (katikati), akipambana kuwatoka wachezaji wa Al Hilal katika mechi ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana. Timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1. **PICHA: MTANDAO**

## Phiri kuongoza 'mauaji'

**Na Adam Fungamwango**

IKISHUKA ugenini kuwakabili wenyeji Primiero de Agosto katika mechi ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa 11 de Novembro, Simba imesema inahitaji na imejipanga kupata matokeo ya ushindi tu.

Mechi hiyo ni ya raundi ya kwanza ya michuano hiyo na timu hizo zinatarajiwa kurudiana Oktoba 16, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Primiero de Agosto walisonga mbele baada ya kuwatoa Red Arrows ya Zambia kwa jumla ya mabao 2-1, ikishinda goli 1-0 ugenini na kulazimishwa sare ya 1-1 wakiwa nyumbani wakati Simba ikiinyuka Nyasa Big Bullets ya Malawi mabao 4-0, mawili katika kila mechi.

Kaimu Kocha Mkuu Simba, Juma Mgunda, alisema maandalizi yote kuelekea mechi hiyo yamekamilika na kinachosubiriwa ni wachezaji wake kufanya kile alichowaelekeza mazoezini huku akifurahia urejeo wa wachezaji waliokuwa majeruhi ambao ni beki, Mohamed Outtara na Sadio Kanoute.

"Majeruhi ni wale wale, Peter Banda, Jimmyson Mwanuke na Shomari Kapombe, lakini furaha niliyonao ni kurejea kwa wachezaji wangu Kanoute na Outtara, wamepona na wapo fiti kwa mechi hii. Niwaambie tu wanachama na mashabiki wa Simba tumemaliza mazoezi vizuri, tunajua, tunafahamu na tunaelewa mechi hii tunayokwenda kucheza ni ngumu, tunakwenda kucheza ugenini, lakini kwa kuelewa hivyo maandalizi ya kwenda kucheza mechi hiyo ngumu yamekamilika," alisema Mgunda.

INAENDELEA UK. 23

# Yanga, Al Hilal hakuna mbabe

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

### Mayele aendeleza makali ya kutikisa nyavu katika michuano ya CAF ingawa...

YANGA imekubali kulazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Al Hilal katika mechi ya kwanza ya raundi ya kwanza ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana.

**Mkongomani Fiston Mayele ambaye ameendelea kuwa na wakati mzuri aliifungia Yanga bao dakika ya 50 lililowaamsha mashabiki wa timu hiyo waliokuwa kimya kwa muda mrefu lakini Mohamed Yousif aliisawazishia Al Hilal na kuifanya mechi hiyo izaliwe upya.**

Mayele alifunga bao hilo baada ya kupenyezewa pasi na Khalid Aucho ambaye alimnyang'anya mpira beki mmoja wa Al Hilal katika eneo la katikati ya uwanja.

Akiwa katikati ya msitu wa mabeki wa timu pinzani, straika huyo aligeuka na kuachia shuti la juu ambalo lilionekana kumparaza beki mmoja wa timu hiyo, ukimpoteza maboya kipa, Ali Abueshrein, na ukajaa wavuni.

Wapinzani hao walisawazisha dakika ya 17 baadaye ambapo wachezaji wa Yanga wakiwa kwenye pilikapilika ya kushambuliwa, mpira uliokolewa na kupigwa ndefu kwa mchezaji hatari aliyeingia kipindi cha pili, Yasir Muzamir ambaye aliambaa na mpira kwenye winga ya kushoto, akapiga krosi ambayo ilishindwa kuzuiwa na Dickson Job na Yousir hakufanya ajizi, akaukwamishwa wavuni.

Kwenye mechi hiyo iliichukua Yanga sekunde ya 49 tu kufika langoni mwa wageni wao, baada ya Bernard Morrison kuwaacha walinzi wa timu hiyo na kumiminia krosi ambyo iliokolewa na Imoro Ibrahim kabla haijamfikia Mayele aliyekuwa amejindaa kuukwamisha wavuni.

Almanusura Mayele aipatie bao Yanga dakika ya 11, baada ya kupiga shuti lililombabatiza kipa. Shuti hilo lilitokana na mpira wa krosi uliopigwa na Jesus Moloko ambaye alidunda kwenye eneo la hatari na kuzua kizaazaa hicho.

Dakika tatu baadaye, mpira wa faulo ya Stephane Aziz Ki ilitua kichwani mwa Morrison ambaye alipiga kichwa mpira ukatoka nje. Morrison, ambaye alionekana kuwasumbua mabeki wa pembeni wa Al Hilal, aliupata tena mpira kwenye winga ya kushoto, alimwacha Altayeba na kupiga krosi iliyomkuta Mayele ambaye alipiga kichwa mpira lakini ukapaa juu ya lango wa wapinzani wao dakika ya 22.

Dakika ya 41, kipa Abueshrein alifanya kazi ya ziada alipopangua kwa ustadi shuti kali la mbali lililopigwa na Stephane Aziz Ki, kabla ya kuwa kona ambayo haikuzaa matunda. Katika mechi hiyo kila timu ilitawala kipindi moja, Yanga ikitawala zaidi kipindi cha kwanza na wageni wakibadilika kabisa kipindi cha pili baada ya kutofanya shambulizi lolote kwenye dakika 45 za kwanza.

Kipa wa Yanga, Djigui Diarra alifanya kazi ya ziada baada ya kudaka mara mbili mipira ikiwa katika miguu ya washambulizji wa Al Hilal kwenye dakika nne za nyongeza na kuiokoa Yanga kuadhirika nyumbani.

**MUCHACHO AONYESHA UZALENDO**

Shabiki maarufu wa Simba, Said Muchacho akiwa katika jukwaa la watu maalum na amevalia jezi yake ya Wekundu wa Msimbazi alionyesha uzalendo kwa kuwahamasisha mashabiki wa Yanga kushangilia timu yao.

Muchacho alionekana kila mara kuwataka mashabiki wa Yanga waliofika uwanjani hapo kutokaa kimya na badala yake kuwahamasisha wachezaji wao kuendelea kupambana kusaka matokeo chanya.

Hata hivyo licha ya kufanyika kwa hamasa mbalimbali, mashabiki wa Yanga jana walishindwa kuujaza Uwanja wa Benjamin Mkapa kama ambavyo waliombwa na wachezaji pamoja na mabosi wa klabu hiyo.

Hata hivyo, hadi ilipofika saa 8:59 mchana, mashabiki waliofika wakiwa wamevaa

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042